SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Uamuzi** mdogo kesi ya Mbowe kujulikana leo

UKURASA 4



**BENZEMA APIGA BAO LA 300 REAL MADRID**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatatu Januari 10, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579821

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Kipenga mbio U-spika

● **CCM** kuanza mchakato, yataja vituo...

*Endelea ukurasa 2*




## Kilio bei ya mahindi kupaa

UKURASA 3



## Mtazamo wa wadau Baraza la Mawaziri

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, YANGA ZAANZA KUTAFUTANA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6



Katibu wa Idara ya Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu mchakato wa kumpata mgombea wa U-spika, jana jijini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM yapuliza kipenga u-Spika

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi kimepuliza kipenga cha kinyang'anyiro cha kumsaka Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa Spika wa Bunge hilo, Job Ndugai, aliyejiuzulu Alhamisi iliyopita.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi kuu za CCM, mjini hapo, Katibu Idara ya Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Shaka Hamdu Shaka, alisema mchakato wa kumpata mgombea atakayechaguliwa na wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uchukuaji wa fomu utaanza leo hadi Januari 15 ambayo itakuwa siku ya mwisho ya kurudisha fomu.

Alisema mchakato huo utafanyika Makao Makuu ya Chama Dodoma, ofisi ndogo ya CCM Lumumba, Dar es Salaam na Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui, Zanzibar.

Shaka aliwataka wanachama wa chama hicho wenye sifa kwa mujibu wa Katiba kujitokeza kugombea nafasi hiyo.

Alisema baada ya uchukuaji na urejeshaji fomu kukamilika, Januari 17, mwaka huu sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya chama hicho itakutana kwa ajili ya kujadili wagombea na kuishauri Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa wagombea waliojitokeza kuomba kiti cha uspika.

Alisema Januari 18 hadi 19, kutakuwa na kazi ya kuchuja na kufanya uteuzi wa mwisho na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu itafanya kazi hiyo.

Alisema Januari 21 hadi 30, mwaka huu Kikao cha chama cha wabunge wa CCM (Caucus), kitapiga kura kumpata mgombea ambaye atakwenda kusimama bungeni kwa ajili ya kuomba kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kwa mnasaba huo nichukue fursa hii kuwataka Watanzania wote ambao wanakidhi vigezo kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania na kwa mujibu wa Katiba ya CCM wana nafasi na wana fursa kujaza nafasi hii ya uspika," alisema.

Vile vile, Shaka alisema CCM ipo salama na imara chini ya Mwenyekiti Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kitabu cha historia ya CCM kina matukio makubwa ya kusisimua na kwa nyakati zote chama hicho kimekuwa kikipita katika mawimbi, mitikisiko, dhoruba, lakini kamwe hakijawahi kutetereka wala kuyumba ikimaanisha kuwa kipo madhubuti na chama kikubwa cha siasa kilichokomaa Tanzania na Afrika kwa ujumla.

"Hili ambalo lililotokea la kujiuzulu Spika wa Bunge eti ni sehemu ya CCM kutokea mpasuko, hakuna kitu kama hicho hili sio jambo la kwanza kutokea," alisema Shaka.

Alisema kama mpasuko ndani ya CCM, ungetokea mwaka 1984 wakati kulitokea jambo kubwa la kihistoria uliondoka mhimili mkubwa wa Rais wa Zanzibar, Makamu wa Rais na Mjumbe wa Kamati Kuu, hayati Aboud Jumbe, na mwaka huohuo aliyekuwa Waziri Kiongozi, Ramadhan Haji, aliachia ngazi na CCM ilibaki kuwa imara na madhubuti.

Shaka alisisitiza, kujiuzulu kwa Ndugai sio jambo la kwanza kwa sababu hayati Maalim Seif Sharif Hamad na jopo lake waliachia ngazi wakati akiwa Waziri Kiongozi na Mkuu wa Idara za CCM akiwa na viongozi wenzake saba, waliondoka na chama kilibaki kuwa imara.

"Kitabu cha historia ya CCM ukikitazama kwa harakaharaka unaweza ukasema CCM imemalizika, lakini nataka niwambie kuwa CCM kumalizika kwa jambo moja ni kuja kwa nguvu mpya za kujipanga ili kwenda vizuri zaidi."

Hayo yote, alisema yamefanyika wakati demokrasia haijakomaa, lakini sasa imekomaa na kwa nafasi hiyo ya u-Uspika atapatikana mwana CCM mzuri kabisa.

Alisema CCM haina uhaba wa viongozi kwa sababu ndani ya chama hicho viongozi wanaandaliwa, wanapikwa na wana utayari na ndiyo uimara wa chama.

"Chama kingekua dhaifu kingekosa viongozi wazuri mfano mzuri ni Rais Samia ambaye amelILetea taifa heshima kubwa."

Akizungumzia kuhusu uchaguzi wa chama ambao unatarajiwa kufanyika mwaka huu, alisema kitafuata Katiba na kanuni za kuwapata viongozi ndani ya chama na kitakachoangaliwa ni sifa na uwezo wa mtu bila ya uonevu.

# Mtazamo wa wadau Baraza la Mawaziri

**Na Beatrice Shayo**

WADAU wametoa maoni tofauti kuhusu Baraza jipya la Mawaziri, huku wakipongeza kuongezeka idadi ya wanawake na pia mtazamo wa kisiasa kwa mawaziri walioachwa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wadau mbalimbali wakiwamo wasomi na wanasiasa, walisema walioteuliwa ni wakati wao sasa wa kufanyakazi kwa bidii kuhakikisha wanawatumikia Watanzania katika kuleta maendeleo.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. Richard Mbunda, alisema mabadiliko yamezua taharuki ya kisiasa katika jamii kwa sababu yamewaachia maswali wananchi.

"Kwenye hotuba yake Rais Samia Suluhu Hassan, alisema kwamba kuna watu wanapigana vikumbo kwa ndoto za urais mwaka 2025 ndani ya chama, hivyo atawapumzisha ili wakajipange vizuri huko nje," alisema na kuongeza;

"Taharuki ya kisiasa ni watu wanajiuliza mawaziri walioachwa ni miongoni mwa watu waliokuwa wana utaka urais 2025? Hii ni taharuki kubwa na mijadala mingi inajaribu kujielekeza huko."

Aidha, alisema Rais ameamua kuangalia katika baraza hilo kuweka makundi ambayo yalikuwa yanatumika kwenye awamu ya tano na kuamua kuyaleta pamoja kama kuyaunganisha.

Alisema kuna kundi ambalo liliachwa mwaka 2015 hadi 2020 na sasa ameamua kuwaingiza katika baraza hilo kuona namna gani wanaweza kuleta mafanikio.

Alisema makundi ya wanasiasa wenye ushawishi ambao walikuwa nyuma ya mfumo akiwamo January Makamba na Nape Nnauye, walisahulika katika awamu iliyopita.

"Lakini tumeona anamleta Rais mstaafu Jakaya Kikwete karibu, licha ya Katiba kumpa fursa ya kuwa mshauri wa Rais, lakini anapomteua kijana wake ni kumleta karibu na kwa Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda naye imekuwa hivyo hivyo, unaona kabisa watu ambao wameondoka kwenye 'system' (mfumo) walivyorudishwa kwenye mabadiliko ya baraza," alisema.

Alisema ni kwa kiasi gani pengine uteuzi huo unazingatia mwaka 2025, ili wamwezeshe kuchagulika tena katika uchaguzi ujao.

Mkurugenzi wa Kituo cha Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema baraza jipya la mawaziri wakilitazama kwa mfumo kijinsia wamesogea mbele kwa kupiga hatua moja kwa sababu awali walikuwa mawaziri saba wanawake na kwa sasa wapo tisa.

Alisema hata wizara ambazo wanazisimamia mawaziri hao ni za msingi ikiangaliwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Ardhi, Kazi ni wizara nyeti na wanaziweza.

Kwa mujibu wa Henga, katika baraza hilo kuna sura mpya za vijana wengi, Rais amezingatia hilo kwa kuona vijana wakipewa nafasi bado wana nguvu kubwa kwa kuifanya kazi kwa uweledi.

"Baraza linatia moyo namsihi mama wakati mwingine angalau tupate asilimia 50 kwa 50 kwa wakati mwingine itakapobidi kuongeza mawaziri au kubadilisha baraza," alibainisha. Alisema kwa sasa wapo asilimia 36 wamevuka viwango vya umoja wa mataifa na watakapofika asilimia 50 kwa 50 watafikia viwango vya SADC.

Rais Samia, alifanya mabadiliko ya baadhi ya mawaziri kwa kuwaacha na kuwateua wapya.

Mabadiliko hayo yamekuja siku chache baada ya kutangaza kusudio hilo, mwishoni mwa wiki, Ikulu, jijini Dar es Salaam.

Alhamis iliyopita, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliamua kuandika barua ya kujiuzulu wadhifa huo, baada ya kutokea taharuki kufuatia kauli yake ya kupinga mikopo inayopewa Tanzania.

Kauli hiyo ilisababisha hali ya hewa kuchafuka huku baadhi ya wadau wakiwamo wanasiasa, wachumi kumtaka ajiuzulu.

Rais Samia, alisema huenda hilo ni vuguvugu la joto la 2025 na kuahidi kuteua watu atakaoenda nao sawa katika kuleta maendeleo ya Watanzania.

## HABARI KITAIFA

# Bei ya mahindi haikamatiki nchini

**Na Waandishi Wetu**

BEI ya mahindi katika masoko mbalimbali mikoa ya Kanda ya Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara), haikamatiki huku bidhaa hiyo ikianza kuadimika.

Baadhi ya wakazi wa mikoa hiyo waliozungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wameiomba serikali kupitia Wizara ya Kilimo, kupeleka haraka mahindi ya bei nafuu yaliyohifadhiwa katika Ghala la Taifa la Chakula (NRFA).

Uchunguzi wa Nipashe katika mikoa hiyo umebaini kupanda kwa bei ya mahindi kwa uwiano tofauti.

Kupaa kwa bei hiyo kulianza kutikisa tangu mwishoni mwa mwaka jana, kutokana na kupungua sokoni.

Katika masoko ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Sanya Juu (Siha), Sadala (Hai), Mbuyuni na Soko la Kati (Moshi Mjini), gunia moja lenye ujazo wa kilogramu 100 limepanda kutoka Sh. 55,000 hadi 105,000.

Baadhi ya wafanyabiashara wa nafaka akiwamo Willson Tesha, alisema kupanda kwa bei ya mahindi kumechangiwa zaidi na uhaba wa mvua za wakati wa msimu wa vuli.

Mfanyabiashara Lelo William, alisema kupanda kwa bei ya mahindi ni neema, kwa kuwa hayakuwahi kupanda kwa muda mrefu.

Katika Manispaa ya Moshi, mahindi lishe, gunia la kilogramu 100 linauzwa kwa Sh. 127, 000.

Wajasiriamali wanaouza unga katika manispaa hiyo, walisema licha ya bei hiyo kuumiza walaji, wamelazimika kupandisha unga wa mahindi kutoka Sh. 1,000 kwa kilogramu moja hadi Sh. 1,300 kwa kilogramu ya unga wa dona.

Wakati katika Wilaya ya Longido mkoani Arusha, maeneo mbalimbali bei ya mahindi imepanda kwa gunia la kilogramu 100 likiuzwa kwa Sh. 100,000, huku wachuuzi wakilalamikiwa kuhujumu vipimo.

Mmoja wa wakazi wa Engarenaibor, Wilaya ya Longido, Lazaro Kazimito, alisema mahindi hayauzwi kwa kilogramu hivi sasa katika masoko wilayani humo, isipokuwa wafanyabiashara wa nafaka, wanayauza kwa kutumia vipimo vya debe na galoni.

Alisema pamoja na kuwa wachuuzi wanatumia debe na galoni, bado wanawahujumu kwa kuchakachua vifaa hivyo ili viweze kusinyaa na kupunguza kipimo, na wengine hukata debe chini na kuchomelea upya ili kupunguza ujazo.

Alisema wakati mwingine, wachuuzi hao huvalisha debe ndani ya jingine ili kuchukachua ujazo, huku fedha ya ununuzi ikiwa kubwa kulinganisha na vipimo vya mahindi hayo.

Diwani wa Mundarara, Alais Mushao, akizungumzia mfumuko huo wa bei, alisema kila wiki mahindi yamekuwa yakipanda, na kwa wiki iliyopita katika soko la Mundarara, gunia moja lilikuwa likiuzwa kwa Sh. 80,000.

Mmoja wa kinamama wanaoishi Mundarara, Sereya Lukumay, alisema hali ni mbaya na kinachowasaidia kwa sasa ni mchanga wanaopewa kutoka katika mgodi wa madini ya Rubi wa Sendeu, ambao wakichekecha hupata madini na kuuza ili kupata fedha ya kununua chakula na pumba kwa ajili ya mifugo.

Kutokana na ulanguzi huo, Mbunge wa Longido na Naibu Waziri wa Madini Mteule, Dk. Steven Kiruswa, alisema wafanyabiashara wengi wametumia fursa ya ukame kuuza mahindi kwa bei ghali, kwa kuwa kila alipotembelea na kuzungumza na wananchi, walikuwa wanamweleza ongezeko la bei ya mahindi sokoni.

Katika Mkoa wa Manyara, bei ya mahindi haijapanda kama yalivyo maeneo mengine, licha ya kuwapo kwa ukame kwenye maeneo mengi ya mkoa huo.

Mfanyabiashara mkubwa wa mahindi ndani na nje ya nchi, mkazi wa Katesh, Wilaya ya Hanang' Clement Fissoo, alisema kilogramu moja ya mahindi kwa Manyara inauzwa Sh. 600, Arusha Sh. 650 na nchi jirani ya Kenya inauzwa Sh. 720.

Alisema katika Mkoa wa Manyara, ananunua gunia moja la kilogramu 100 kwa Sh. 57,000 hadi Sh. 58,000.

Kadhalika katika Mkoa wa Arusha, wafanyabiashara wa nafaka hasa mahindi, wanalia uhaba wakisema hayapatikani na yanayopatikana yanauzwa bei ya juu, kiasi cha kushindwa kufanya biashara hiyo.

Idrisa Hamisi, mfanyabiashara wa mahindi ya jumla, alisema kwa sasa wanalazimika kununua gunia la kilogramu 100 kwa Sh. 62,000 na kuuza Sh. 650 kwa kilogramu moja.

Alisema upatikanaji wa bidhaa hiyo ni wa shida na wachache walioihifadhi katika maghala wanauza kwa maringo.

Mkulima Sifael Meshaki, mkazi wa Nadosoito, Kata ya Murieth, jijini Arusha, alisema kwa sasa mahindi ni adimu na aliyonayo, anauza gunia moja lenye ujazo wa kilogramu 100 kwa Sh. 75,000.

Kadhalika, katika Wilaya ya Arumeru, baadhi ya wananchi wameiomba serikali kuchukua hatua kudhibiti mfumuko huo wa bei, kutokana na eneo hilo kupanda bei ndani ya wiki moja kutoka Sh. 63,000 hadi Sh.70,000.

■ **Imeandikwa na Zanura Mollel, Tumaini Mafie, Cynthia Mwilolezi (Arusha), Jaliwason Jasson (Manyara), Mary Mosha (Moshi)**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**
**TALAKA 01/2022**

**MDAI…………FIRST BATINO MHALUKA**
**DHIDI**
**MDAIWA.GODFREY GUSTAFU KISWEKA**

**MAOMBI YA TALAKA**

Unatakiwa kufika mahakama tarehe 17/01/2022 saa 2:30 asubuhi kwa ajili ya shauri la talaka usipofika shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 07/01/2022.

…………………
**HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**



**Bank of India (Tanzania) Ltd.**

*Relationship beyond banking*

**DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019**
**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

| NO. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Current Accounts** | | |
| a) | Required minimum opening balance | 500 | 500,000 |
| b) | **Monthly service fee (breakdown per customer)** | | |
| | Folio Charge | 4 | 6,000 |
| c) | Cheque withdrawal over the counter | | |
| | **Up to** Tshs 25,000,000 a day | - | free |
| | **Over** Tshs 25,000,000 a day | - | 0.15% of withdrawn amount |
| | **Up to 5000 USD a day** | free | - |
| | **Over 5000 USD withdrawal** | 0.6% of withdrawn amount | - |
| d) | Fees per ATM withdrawal | - | - |
| e) | ATM mini statement | - | - |
| f) | Interim/additional statement per page | 1.50 | 1500 |
| g) | Periodic scheduled statement | free | free |
| h) | Cheque book **(50 leaves)** | 27 | 42,000 |
| i) | Dishonoured Cheque | 55 | 70,000 |
| j) | Special clearance | | |
| | Within walking distance 1km | 45 | 70,000 |
| | More than 1km | 65 | 95,000 |
| k) | Counter cheque | - | - |
| l) | Inward/Outward cheque collection-USD | 0.60% Min comm. 18 postages USD 90 | - |
| m) | Cancelation of bankers cheque/DD | 15 | 20,000 |
| n) | | | |
| o) | Stop payment | 28 | 35,000 |
| p) | Standing order | - | - |
| q) | Balance enquiry | free | Free |
| r) | Issue of Balance certificate | 7 | 9,000 |
| s) | New ATM card issuance | - | - |
| t) | ATM card renewal or replacement | - | - |
| u) | Overdrawn account interest charge | - | - |
| | - Overdrawn in current account | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| | - Overdrawn in loan account | 2% over regular rate | 2% over regular rate |
| | - Unarranged overdraft | 2% over the TOD rate | 2% over the TOD rate |
| v) | Interbank transfer | - | - |
| w) | Bill payments through ATM | - | - |
| x) | **Deposit fee** | - | - |
| | **Savings Accounts** | | - |
| | (Up to USD 5000) | Free | - |
| | (Over USD 5000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |
| | **Current account.** | | |
| | (Up to USD 10000) | Free | - |
| | (Over USD 10000) | 0.6% of deposited amount | - |
| | Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both below and above USD 5000) | 12% (Min USD 1) of the aggregate of small currency amount | - |

| No | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE USD | CHARGE/FEE TSHS |
|---|---|---|---|
| 2.0 | **Savings Accounts** | | |
| a) | Saving bank customer ID Card-one time | 7 | 10,000 |
| b) | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 2,000 | 25,000,000 |
| c) | Cash withdrawal charges over USD 2,000 to 5,000 per day | 0.25% of withdrawal amount | |
| d) | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.60% of withdrawal amount | |
| e) | Cash withdrawal charges over TZS 25,000,000 per day | | 0.10% of withdrawal amount |
| f) | Required minimum opening balance | | |
| | Without Cheque book | 50 | 50,000 |
| | With Cheque book | 200 | 200,000 |
| g) | Monthly service fee | - | - |
| h) | Interim statement | 1.5 per page | 1500per page |
| i) | Cheque book charges 25 leaves | 15 | 20,000 |
| j) | Account closure | 25 | 35,000 |
| k) | **Maintenance of minimum account balance** | | |
| | Without cheque book | 50 | 50,000 |
| | With cheque book | 200 | 200,000 |
| l) | **Minimum balance charges (in case of non maintenance of minimum balance )** | | |
| | Without cheque book | 4 p.m | 900 p.m |
| | With cheque book | 15 p.m | 3,600 p.m |
| 3.0 | **Current Accounts** | | |
| | Ledger folio charges per folio (40lines per folio) | 4 per folio | 6,000 per folio |
| | Cash withdrawal per day-Free of charge up to amount | 5,000 | 25,000,000 |
| | Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | 0.6% of withdrawal amount | - |
| | Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | | 0.15% of withdrawal amount |
| | Cheque book charges 50 leaves | 27 | 42000 |
| | Account closure charges | 70 | 85,000 |
| | **Maintenance of minimum account balance** | 500 | 500,000 |
| | **Minimum balance charges** | 15 p.m | 20,000 p.m |
| 4.0 | **Electronic Banking** | | |
| a) | Internet banking monthly fee | - | - |
| b) | Internet transfers | - | - |
| c) | SMS banking | - | - |

| No | ITEM/TRANSACTION | Minimum SMS Alert Charge ( to be recovered quarterly upfront) | Number of Free SMS on paying SMS Alert charge | SMS Alert charge per SMS beyond the free SMS (To be recovered in monthly basis) |
|---|---|---|---|---|
| d) | SMS Alert facility - | | | |
| | - **Individual** | free | free | Free |
| | - **Corporate** | free | free | Free |

| No | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| e) | Others | - | - |
| 5.0 | **Foreign Exchange Transaction.** | - | - |
| a) | Purchase/sale of TCs transactions over the counter | - | - |
| b) | Purchase of foreign Cheque. | - | - |
| c) | Sale/purchase of cash passport. | - | - |
| d) | Telegraphic transfer. | | |
| | Remittances Outward(TISS) | 10 | 10,000 |
| | Other Outward remittances: | | |
| | | A/C holder / Non A/C holder | |
| | Up to USD 6,000 | 15 / 40 | – |
| | USD 6001-10,000 | 30 | – |
| | Above USD 10,000 | 0.35%max USD 210 | – |
| e) | Telex/SWIFT. | 30 | - |
| f) | Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank). | | |
| 6.0 | **Other Charges** | | |
| a) | Activation of Dormant Accounts - Per Activation | | |
| | - **Individuals** | 3 | 5,000 |
| | - **Corporate** | 6 | 12,000 |
| 7.0 | **Personal Loans. Charges** | | |
| a) | Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| i) | Personal loans | 1.50% | 1.50% |
| ii) | Overdrafts | 1.50% | 1.50% |
| iii) | Mortgage finance | 1.50% | 1.50% |
| iv) | Asset finance | 1.50% | 1.50% |
| b) | Unpaid loan instalment | 5.00% Over the applicable rate | |
| c) | Early repayment | 2.5% of prepaid loan amount | |
| d) | Valuation fees | As per actual charges by valuer | |
| e) | **Others** | | |
| i) | Documentation charges | Actuals as per advocate bill | |
| ii) | Document Handling Charges | 0.30% of loan amount | |
| iii) | Inspection Charges | Tshs 30,000 per visit | |
| iv) | Modification charges | 0.25% on the sanctioned limit | |
| 8.0 | **Guarantee (Performance/Financial)** | | |
| | Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part there of minimum for one quarter | |
| | Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| 9.0 | **Imports** | | |
| | LC opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | |
| | LC amendment charges | Per amendment 0.40% of LC mount (minimum USD 60 and maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (same for LC against 100% cash margin) | |
| | Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 180 | |
| | Retirement of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Inward Bills for collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |
| 10.0 | **Exports** | | |
| | Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |
| | Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30 | |
| | LC advising charges | USD 150 | |
| | Export Bills for collection | 0.60% of Bill amount minimum USD 30 maximum USD 360 | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 05.01. 2022 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 05.01. 2022 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 05.01. 2022 |

**OTHER DISCLOSURES**
**(VIAMBATANISHI NYINGINEZO)**

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| 1.0 | **Base or Prime Lending rate** | 7.00% p.a. | 14.00% p.a. |
| 2.0 | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| 3.0 | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| 4.0 | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 5.75% |
| | Over 6 months | 2.50% | 6.75% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.00% | 7.25% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| No. | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 05.01. 2022 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 05.01. 2022 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 05.01. 2022 |

# HESLB kutoa mikopo ndani ya saa 24

**Na Elizabeth Zaya**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), inatarajia kuanza kuwasajili wanafunzi 70,396 wanufaika wa mwaka wa kwanza katika mfumo wa kidigitali wa malipo ya fedha za mikopo ambao utawawezesha kupokea fedha ndani ya saa 24.

Mkurugenzi wa Upangaji na Utoaji Mikopo HESLB, Dk. Veronica Nyahende, aliyesema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari na kufafanua kuwa usajili huo utajumuisha kuchukuliwa kwa alama za vidole, taarifa za kibenki, picha pamoja na taarifa za usajili wa wanafunzi vyuoni utakoanza leo.

"Mfumo huu unaitwa 'Digital Disbursement Solution' maarufu kama DiDiS na tuliuanzisha mwaka 2018, ili kurahisisha fedha kuwafikia wanafunzi kutoka siku 10 hadi saa 24 hivi sasa," alisema, Dk. Nyahende.

Aliwakumbusha wanafunzi wote wa mwaka wa kwanza ambao ni wanufaika wa mikopo hiyo pamoja na wengine ambao wamepata mikopo kwa mara ya kwanza mwaka 2021/2022 kujitokeza ili kusajiliwa.

"Malipo yote ya robo ya tatu kwa mwaka huu wa masomo yatafanyika kupitia mfumo huu, kwa hiyo ni muhimu kwa wanafunzi kujisajili ili wapokee malipo yao," alisema Dk. Nyahende.

"Maofisa wa HESLB watakuwa vyuoni kuanzia Jumatatu, Januari 10 ili kushirikiana na maofisa wa vyuo katika kazi ya usajili, na taarifa za ziada kuhusu maeneo na muda wa usajili yatatolewa katika ofisi za maofisa mikopo wa vyuo husika," alisema Dk. Nyahende.

Alitoa wito kwa viongozi wa serikali za wanafunzi na maofisa mikopo katika vyuo kuwahamasiha wanufaika kujitokeza ili kujiandaa kupokea fedha za malipo ya mikopo bila usumbufu.

"Usajili huu ukifanikiwa, maofisa mikopo wataondokana na usumbufu wa kutunza kumbukumbu kwa karatasi na wanafunzi watakuwa wanapokea fedha haraka na hivyo kutumia muda mwingi kusoma," alisema Dk. Nyahende.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/2022, serikali imetenga Sh. bilioni 570 kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu na zitawanufaisha wanafunzi 168,000.



Vijana waendesha baiskeli wanaosafirisha pombe ya asili aina ya ulanzi kutoka Tanangozi na Ihemi Wilaya ya Iringa wakiwa wameshikilia lori lililokuwa linatembea ili kupata msaada wa mwendo wa haraka barabara kuu ya Iringa -Mbeya juzi, ambayo ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Uamuzi mdogo kesi ya Mbowe leo

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, leo inatarajia kutoa uamuzi mdogo wa kupokea ama kutopokea kielekezo cha sare za Jeshi la Wananchi Tanzania, Jeshi la Kujenga Taifa na ramani za vituo vya mafuta zinazodaiwa kukutwa kwa mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu.

Uamuzi huo utatolewa mbele ya Jaji Joackim Tiganga baada ya kupitia hoja za kupinga majibu ya upande wa Jamhuri yaliyowasilishwa Desemba 20, mwaka jana.

Upande wa utetezi uliweka mapingamizi ya kutopokelewa mahakamani kwa kielelezo namba 14 ambacho ni sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania(JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na ramani za vituo vya mafuta, zilizokutwa na mshtakiwa wa kwanza Halfani Bwire.

Inadaiwa upande wa utetezi wamekosa imani na mnyororo wa kuhifadhiwa vielelezo hivyo hadi kufikishwa chumba cha mahakama.

Kielelezo hicho kiliombwa kutolewa mahakamani na shahidi wa nane wa upande wa mashtaka, Mrakibu wa Polisi (SP), Jumanne Malangahe.

Awali, akijibu mapingamizi, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, alidai katika hoja za upande wa utetezi hakuna hata moja ambayo imeonyesha kuwa upekuzi haukufanyika kabisa au vielelezo vilivyowasilishwa mahakamani ni tofauti na vilivyopatikana wakati wa upekuzi.

Wakili Kidando alidai uwezo na mamlaka ya shahidi kuwasilisha vielelezo mahakamani, waliomba mahakama kuwa shahidi huyo ana mamlaka kwa kuwa ndiye aliyekuwa ofisa mkamataji wa vielelezo hivyo na sio hitaji la kisheria kuwa lazima aonyeshe ujuzi wa utambuzi wa vifaa hivyo vya kijeshi hata kama hakuwahi kufanya kazi katika jeshi, hatua yake ya kukamata tu inatosha kumpa mamlaka ya kuviwasilisha.

"Upande wa mashtaka tunaona hoja za upande wa utetezi hazina mashiko kisheria na hazina msaada kupata suluhu ya kilichopo mahakamani hapo na hivyo tunaiomba mahakama itupilie mbali," alidai Kidando.

Mawakili wa utetezi katika baadhi ya mapingamizi walidai mnyororo wa uhifadhi wa kielelezo hicho shahidi hajauweka wazi hadi kilipofika mahakamani hapo.

Wakili upande wa utetezi, Nashon Nkungu, alidai shahidi huyo ambaye ni askari polisi hakuwahi kuieleza mahakama kuwa na utaalamu wa kuainisha sare za jeshi mbalimbali zikiwamo alizodai ni za JWTZ na JKT alizomkuta nazo mshtakiwa wa kwanza Halfani Bwire.

Wakili wa Nkungu alidai vielelezo hivyo havijathibitishwa kwa namna inayofaa kisheria jambo linaloleta mashaka na kuiomba mahakama kutokuvipokea kwa kukiuka mlolongo wa kisheria.

Nkungu aliendelea kudai hoja ni kwa vipi vielelezo vilitoka chumba cha mashtaka hadi kutua mahakamani kwa kuwa haikusemwa vilikuwa chini ya uangalizi wa nani.

Upande wa utetezi waliiomba mahakama isichukue ushahidi huo kwa kuwa umevunja sheria, kupokea vielelezo hivyo kutokana na askari kuchukua vielelezo bila kufuata sheria na kunavunja haki za wateja wao.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Bwire, Adam Kasekwa na Mohamed Ling'wenya.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kwa kulipua vituo vya mafuta kati ya Mei hadi Agosti 5, 2020.

Mbowe amekula Krismasi na Mwaka Mpya gerezani ikiwa ni mara ya pili, mwaka 2018 alikula sikukuu hizo akiwa gerezani baada ya Mahakama ya Kisutu kumfutia dhamana kwa kukiuka masharti ya dhamana.

# Kampuni yahamasisha wafanyakazi chanjo UVIKO-19

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAFANYAKAZI wa Kampuni ya Ulinzi ya SGA Security (T) mkoani Morogoro wamejitokeza kuchanja chanjo ya kujikinga na virusi vya corona (COVID -19) ili kujilinda wao, familia zao na wateja wanaowahudumia ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali dhidi ya ugonjwa huo.

Kujitokeza kwa wafanyakazi hao kumetokana na uongozi wa kampuni kuendesha zoezi la kutoa elimu na kuhamasisha wafanyakazi, familia zao na wananchi kuchanja chanjo ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona ambazo zimeletwa na serikali.

Muuguzi wa kampuni hiyo, Jesca Pande, alisema hayo mjini hapo, wakati akitoa elimu ya ugonjwa huo na uhamasishaji kwa askari wa kampuni hiyo waliopo mkoani Morogoro kujitokeza kupata chanjo hiyo. Alisema, katika kuunga mkono juhudi za serikali, Agosti 4, mwaka huu (2021), Kampuni ya Ulinzi ya SGA Security (T), ilianza kutoa elimu na kuhamasisha walinzi, wafanyakazi wengine na familia zao kujitokeza kupata chanjo na hadi sasa zaidi ya wafanyakazi 1,100 wamepata chanjo hiyo.

Muunguzi wa kampuni hiyo alisema, tangu kuanza kwa utoaji elimu na uhamasishaji kwa wafanyakazi kuhusu chanjo, tayari imetolewa kwenye ofisi za mikoa ya Tanga, Dodoma, Mwanza, Geita, Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Songwe (Tunduma) na Morogoro.

"Tumepanga kuwafikia wafanyakazi wote wa kampuni yetu kwa Tanzania nzima, kuhamasisha chanjo kwa ajili ya kuwalinda wao wenyewe, familia zao na wateja ili kuwapa huduma bora zaidi," alisema Jesca. Baadhi ya wafanyakazi wa kampuni hiyo waliopata chanjo akiwamo, Donarti Kabwili, Bahati Michael, Erasto Kapinga na Juma Omary, kwa nyakati tofauti waliipongea Kampuni yao kwa kuhamasisha wafanyakazi wake kujitokeza kwa hiari yao kupata chanjo inayotolewa na serikali.

"Tunaomba kila mwenye uelewa ajitokeze kuchanja ili maisha yaendelee, mimi nimechanja ili kujali afya yangu na familia yangu, watu wajitokeze na si jambo zuri kukataa chanjo," alisema Omary.

Kwa upande wake Bahati Michael, alisema wao ni askari na wana wajibu wa kuwa mabalozi wazuri katika mapambano hayo ili waweze kuwahamasisha vyema wananchi waendelee kujitokeza vituoni kupata chanjo hizo ambazo ni salama.

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA UJENZI WA HUDUMA ZA UGAVI WA MAJI KWA MRADI WA EACOP KUMBUKUMBU NA. ECP-21-C-015

KAMPUNI ya Mafuta na Gesi ya TOTAL East Africa Midstream BV (Company) Tanzania, inawaalika wakandarasi wazoefu na wanaoheshimika ambao wana uwezo unaoonekana, uzoefu uliothibitishwa, utayari na uwezo wa kueleza nia yao ya kutoa huduma zifuatazo kwa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. mradi wa EACOP.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Ujenzi wa mifumo ya maji chini ya ardhi / visima kama ifuatavyo:
1.Uchimbaji wa Visima vya Majaribio kabla ya uendelezaji kamili wa visima kwa madhumuni ya uzalishaji
2.Shughuli za Kuchimba visima
- Kuchimba visima vyema kwa kutumia Mashine ya aina ya rotary.
- Rig na njia ya kuchimba visima iliyopitishwa lazima iwe ya kufaa kwa kuchimba visima kupitia nyenzo zisizounganishwa, na mwamba mgumu, uliounganishwa.

3.Ujenzi wa Kisima ni pamoja na lakini sio zaidi ya:
- Ununuzi wa vifaa muhimu: Pampu, casings, mabomba, paneli za jua, tanki la kuhifadhi maji,…
- Ufungaji na uunganisho wa casings na skrini
- Zana na nyenzo zote muhimu kwa ajili ya kufanya shughuli za uvuvi inapohitajika
- Ufungaji wa muhuri wa saruji na pakiti ya Gravel
- Kuua vijidudu na kusafisha kisima
- Vifaa vya Juu ya ardhini (makazi, uzio n.k.)
- Vipimo vyote muhimu: Vipimo vya kusukuma maji, vipimo vya sampuli za maji na udongo, …
- Shughuli zote zitazingatia kanuni za mazingira za Tanzania,
- Shughuli, Rekodi za Kukamilisha na Ripoti

Kazi hiyo itafanywa katika maeneo mbalimbali nchini kote

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Brela ORS, CRB, OSHA na wizara ya maji kama kampuni ya kuchimba visima
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi
- Maelezo ya uzoefu wa siku za nyuma katika kutoa uendelezaji wa visima vya maji: Mashimo ya majaribio, uchimbaji wa visima, ukamilishaji wa kisima, usakinishaji juu ya ardhi,…
- Orodha ya miradi iliyotangulia: maelezo, mteja, eneo,…
- Orodha ya mifumo na vifaa inayomilikiwa, wafanyikazi wenye vigezo na uzoefu
- Maelezo ya kina ya Mitambo ya kuchimba visima : aina, uwezo, vyeti,…
- Maelezo ya mfumo wa afya usalama na mazingira: Mpango wa HSE, taratibu za HSE, rekodi za HSE, mfano wa tathmini ya hatari,..
- Maelezo ya mfumo wa ubora
- Uthibitisho wa uwezo wa kifedha kutekeleza wigo uliopendekezwa wa huduma
- Nakala ya Sera za Kupambana na Rushwa na Maadili

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **adeline.m-mari@external.totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00 mchana** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **24 Januari 2022.** Kichwa cha Barua Pepe ni ECP-21-C-015/EOI

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

EAST AFRICAN
**CRUDE OIL PIPELINE**

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA UHANDISI WA HUDUMA ZA UGAVI WA MAJI KWA MRADI WA EACOP KUMBUKUMBU NA. ECP-21-C-016

KAMPUNI ya Mafuta na Gesi ya TOTAL East Africa Midstream BV (Company) Tanzania, inawaalika wakandarasi wazoefu na wanaoheshimika ambao wana uwezo unaoonekana, uzoefu uliothibitishwa, utayari na uwezo wa kueleza nia yao ya kutoa huduma zifuatazo kwa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki. mradi wa EACOP.

**MAELEZO MAFUPI YA UPEO WA HUDUMA:**
Uhandisi wa maji chini ya ardhi/mifumo yenye msingi wa visima na/au kuunganisha kwa mifumo iliyopo ya mtandao wa maji inajumuisha utafiti wa eneo-kazi, uchunguzi wa tovuti na Uhandisi wa kina. Upeo umefupishwa ndanimaelezoundani hapa chini

**Mifumo ya maji ya ardhini/kisima**
**UFUNZO WA DESKTOP (tie-ins kwa mifumo iliyopo ya mtandao wa maji)**
Kusanya na kukagua nyaraka zozote zilizopo , ikijumuisha: 1/ tafiti za kijiofizikia na hidrojiolojia zilizofanywa mapema na Wizara ya Maji au taasisi nyingine yoyote; 2/ ramani zinazopatikana, picha za angani, ripoti na taarifa zingine za rasilimali maji za visima vilivyochimbwa hapo awali;
Fanya uchunguzi wa upelelezi eneo la ardhi pamoja na :
- hupitia njia za kijiolojia ili kutambua hali ya kijiolojia na hidrojiolojia
- Sensa ya visima vilivyopo, visima vyeye kina virefu, mikondo ya maji na vipengele vya maeneo yenye dalili za maji ndani ya eneo la kilomita 3 la kituo cha usambazaji kinachohitajika (SITE), au eneo linalopendekezwa la ukuzaji wa kisima ikiwa liko mbali na SITE;
- Upimaji wa visima vyeye kina virefu na visima vilivyopo, ikijumuisha kiwango cha maji na vipimo vya msingi vya ubora wa maji;

**Ripoti ikijumuisha**
- Ramani za Hydrojiolojia na Piezometric; ikijumuisha eneo na kina cha visima vilivyopo
- Utafiti wa dhana ya muundo wa kisima (inapowezekana kuifanya kutoka kwa utafiti wa eneo-kazi),
- Mpango wa program za ziada na kina wa uchunguzi unaohitajika kwa muundo wa kisima katika eneo husika.

**Tie-ins kwa mifumo iliyopo ya mtandao wa maji**
**UFUNZO WA DESKTOP (mifumo ya maji ya ardhini/kisima)**
Kusanya na kupitia takwimu zote muhimu kutoka katika mabonde yanayohusika na mamlaka za usambazaji maji kuhusu mtandao wa usambazaji maji uliopo, mfano ukubwa wa mabomba, vifaa vya ujenzi wa mabomba, ubora wa maji n.k.

**RIPOTI ikijumuisha:**
Uchambuzi wa data zote zilizokusanywa katika muktadha na uwezekano wa kuunganishwa kwa mitandao iliyopo ya usambazaji

**UCHUNGUZI WA ENEO**
Uchunguzi wa kijiofizikia kufanywa kwenye maeneo yanayoweza kuchaguliwa yaliyotambuliwa, mahsusi yaliyo chaguliwa na kpendekezwa ili kupata maeneo yenye maji. Ripoti ya uchunguzi wa itajumuisha:
- Programu ya uchunguzi na uhalali wa mbinu zilizochaguliwa za uchunguzi
- Ufafanuzi wa data, ikijumuisha: 1/Aquifer jiometri & sifa za majimaji na kuchaji upya, 2/kemia ya chemichemi na mambo yanayoathiri kemia; 3/ Uwezekano wa kuendeleza rasilimali za maji chini ya ardhi ikiwa ni pamoja na idadi inayotarajiwa ya visima, maeneo, kina, nk.

UBUNIFU WA KINA WA UHANDISI
- Ubunifu wa Kisima cha Maji, Bomba la Kisima cha Maji, Bomba, vifaa na vifaa vinavyozunguka, Hifadhi ya Maji,…
- Michoro ya kina, vipimo vya kiufundi

**UCHUNGUZI WA ENEO**
- Kutembelea maeneo ili kuimarisha mtandao uliopo katika eno husika kuzingatia eneo la kazi;
- Tathmini ya hali ya miundombinu iliyopo yaani hali ya bomba, pampu za nyongeza nk.
- Kuanzisha maeneo yanayowezekana kwa ajili ya kuunganisha;
- Sampuli na uchambuzi wa ubora wa maji
- Kufanya uchunguzi wa Topografia kwa njia za bomba
- Ripoti ya uchunguzi itakayo jumuisha taarifa pamoja na habari hapo juu

UBUNIFU WA KINA WA UHANDISI
- Kubuni mtandao kutoka eneo la mfumo mpaka eneo la kazi na pia kwa kuzingatia mifumo ya majumbani katika maeneo ya wananchi/jamii;
- Michoro ya kina, vipimo vya kiufundi

  Kazi hiyo itafanywa katika maeneo mbalimbali nchini kote

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:
- Uthibitisho wa kusajiliwa na Brela ORS na CRB.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Maelezo ya uzoefu wa zamani katika kutoa uhandisi wa usambazaji wa maji: Uendelezaji wa kisima na/au kuunganishwa na mtandao uliopo wa maji.
- Orodha ya miradi iliyotangulia: maelezo, mteja, eneo,…
- Orodha ya vifaa na mifumo inayomilikiwa, wafanyikazi waliohitimu na wenye uzoefu
- Uthibitisho wa uwezo wa kifedha kutekeleza wigo uliopendekezwa wa huduma
- Maelezo ya mfumo wa afya usalama na mazingira na sera ya Ubora
- Nakala ya Sera za Kupambana na Rushwa na Maadili

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **adeline.mmari@external.totalenergies.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **24 Januari 2022.** Kichwa cha Barua Pepe ni ECP-21-C-016/EOI.

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viwanja vya CCM kuwekwa nyasi bandia mbona kimya?

**JUNI** mwaka jana, Bunge lilipitisha pendekezo la serikali la kusamehe kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye nyasi bandia kwa viwanja vya mpira wa miguu katika majiji ili kuendeleza michezo na kukuza vipaji nchini.

Ni wakati Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba alipokuwa akiwasilisha mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/22 Bungeni Dodoma kwa ajili ya kujadiliwa.

Nchemba alisema viwanja vingi ni vibovu sana na ubovu wa viwanja hivyo unasababisha baadhi ya timu kutopata matokeo mazuri zinapokwenda kucheza hususan mikoani.

Ikasemwa kuwa mpango huo ukikamilika, basi kwenye bajeti ya msimu huu au misimu ijayo, serikali inaweza kuangalia suala la msamaha hata kwenye mikoa, wilaya na sehemu zingine.

Lakini Nipashe tunaona kimya kikizidi kutawala katika utekelezaji wa mpango huo wa nyasi bandia, kwani tangu msamaha huo kutolewa hakuna juhudi zozote zimeonekana kuendelea hadi sasa.

Wadau wa soka hususan Kampuni ya Azam Media, imekuwa ikifanya marekebisho ya viwanja kwa kuweka taa, na tayari Uwanja wa Jamhuri Dodoma ukiwa umefungwa taa, huku wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi ukiendelea na matengenezo hayo, mchakato ambao tulidhani ungeenda sambamba na uwekaji wa nyasi bandia viwanjani.

Tunakumbuka hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, aliwahi kuongelea kuhusu suala la ubovu wa viwanja ambavyo vingi vinamilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), akikitaka kurekebisha viwanja vyake na kama hakiwezi, basi waangalie jinsi gani ya kuingia makubaliano na wawekezaji.

Hii inaonyesha kuwa serikali ya Tanzania chini ya Rais Samia bado ina nia nzuri na soka katika kuendeleza soka la nchi hii, lakini inaonekana kuna tatizo mahala, ambalo linahitaji kutatuliwa ama kushughulikiwa ili mambo yaende sawa.


Tunaamini bado kuna baadhi ya watendaji ndani ya chama hicho wenye fikra potofu kwamba michezo ni burudani, afya, upendo, kufahamiana na kudumisha undugu pekee, bila kutambua ni ajira kubwa duniani na inaweza kutua fursa pana kwa vijana kujiajiri na kupunguza mzigo kwa serikali.

Kama hiyo haitoshi, michezo pia kwa sasa inazipatia serikali nyingi mapato mengi kuliko hata baadhi ya kampuni, lakini ni sehemu ambayo inatoa ajira kwenye nyanja nyingi, ikiwamo wanamichezo, wafanyabiashara, makocha, madaktari, waunguzi, mama lishe, machinga ambao wanauza jezi na kadhalika, hivyo suala la ubora wa viwanja haliepukiki kwa sasa.

Tulitegemea hadi leo hii, hata kama nyasi za bandia hazijafika, lakini wadau wa soka wangekuwa wameshapewa mrejesho kuwa yale yaliyotamkwa na rais huku pia yakipitishwa bungeni dalili za utekelezaji zingeonekana, lakini wapi!

Inasikitisha kuona Ligi Kuu Tanzania Bara ikizidi kupata sifa ndani na nje barani Afrika huku wachezaji wengi wakivutiwa kuja kucheza nchini hadi Ligi Daraja la Kwanza (Championship), lakini viwanja vikiendelea kulitia doa soka letu kila uchao ndiyo maana tumeona ipo haja ya kuwakumbusha tena wamiliki wa viwanja hivyo kuna umuhimu wa kuvifanyia maboresho hayo mapema kupitia msamaha huo wa VAT kwa nyasi bandia.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tatizo vipaji vya soka Zanzibar ni hili tu...

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara nyingine tena tumeona vipaji halisi vya wachezaji wengi wa Zanzibar kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi inayoendelea. Hii si mara ya kwanza wala ajabu kuona vipaji vya hali ya juu kwa wachezaji Zanzibar.

Zanzibar kwenye soka ni kama mikoa yenye madini ambayo hata mvua ikinyesha, ukichukua mchanga na kwenda kuuchekecha unaweza kupata. Haijawahi kuishiwa.

Mwaka huu kwenye Kombe la Mapinduzi kulikuwa na timu za Selem View, Taifa Jang'ombe, Mlandege, KMKM, Meli Nne City na Yosso Boys ambazo ukiziangalia utakutana na wachezaji wengi wenye uwezo wa hali ya juu wa kumiliki mpira, kupiga chenga na mengine mengi yanayotokana na misingi halisi ya soka.

Utashangaa kuona timu hizo zote za Zanzibar zimetoka na kubaki za Tanzania Bara. Ni kweli na hii inatokana na aina tofauti ya soka linalochezwa.

Wachezaji wa Zanzibar, wana vipaji na kucheza soka la kufundishwa, lakini wanakosa mwendelezo wa mafunzo ya soka la ushindani, kutafuta matokeo na nguvu pia.

Kifupi ni kwamba wachezaji wa Zanzibar kutokana na kujifahamu kuwa wana vipaji, wanacheza soka la kishule zaidi ambapo wanafurahia sana kupiga chenga, kanzu, kupasiana zaidi, kuliko kusaka matokeo.

Ndiyo maana utaona hata timu yao imeshafunga mabao mawili au matatu, lakini wataendelea kucheza vile vile na huwa huoni uharaka wa wao kuharakisha kwenda mbele kusaka ushindi.

Makocha wa Zanzibar, akiwamo wa Meli Nne City ya Zanzibar Ally Omari, alisema moja ya tatizo la wachezaji wa Zanzibar ni kwamba hawana nguvu za kutosha za kupambana kutokana na kupenda sana vyakula aina ya chips.

"Wenzetu Bara wachezaji wana ratiba nzuri ya kula na kusimamiwa ipasavyo, hivyo lazima wawe bora, maana wanapata huduma zote," alisema kocha huyo.

Makocha Zanzibar wamekuwa wakilalamika kuwa kambini wachezaji hao wamekuwa wakipikiwa ugali na wali na mboga ya samaki, lakini wao wamekuwa wakipenda kula chips. Ukiangalia kuna ukweli kuhusu hilo, kwani kuna utofauti kati ya wachezaji wa Kizanzibar na Bara.

Wakati wachezaji wa Zanzibar wakiwa na ufundi zaidi na misingi ya awali ya soka, wachezaji wa Bara msingi wao zaidi ni nguvu, pamoja na kujua nini kinatakiwa kufanyika na kwa wakati gani.

Wachezaji wa Bara hawana ufundi sana kama Wazanzibar, lakini wakiwa uwanjani wanaonekana wanacheza kwa sababu gani na nini wanakitaka.

Ndiyo maana utaona hata timu ya Zanzibar iwe nzuri vipi kuliko ya Bara, lakini wanaweza kukosa matokeo kutokana na jinsi wanavyocheza kwa maonyesho zaidi kuliko kusaka ushindi, mchezo ambao mara nyingi huchezwa kwenye shule za msingi zaidi.

Ina maana kama kutakuwa na juhudi za makusudi za kuwasaidia wachezaji wa Zanzibar kwa kuwapa mafunzo zaidi, taifa linaweza kupata wachezaji wazuri zaidi ya hawa tulio nao.

Kwa uchezaji ule wa Zanzibar, halafu wachezaji wakajua jinsi gani ya kusaka ushindi, huku wakiwa wamejazwa stamina na pumzi, timu zao zinaweza kuwa ni hatari sana. Tangu zamani tumeona wachezaji kutoka Zanzibar walivyotamba sana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kupata ladha ya ushindani wa soka huko.

Wachezaji kama kina Innocent Haule, Hamisi Machungwa, Thuwein Ally, Abdi Kassim, Nadir Haroub 'Cannavaro', na sasa Feisal Salum. Hawa ni wachache waliopata nafasi ya kuvuka maji kwenda Bara na wakafanikiwa kufanya makubwa kwenye timu za huko na Taifa Stars.

Hii ina maana kuwa nchi inapoteza wachezaji wengi ambao hawapati nafasi yoyote ya kutoka Zanzibar. Vipaji vinafia huko huko. Nadhani sasa umefika wakati kwa wavumbuzi wa vipaji na shule za kuvilea kuiangalia Zanzibar kama sehemu ambayo ni mgodi wa dhahabu. Wanachotakiwa kufanya ni kwenda kuweka viwanda huko kwa ajili ya kuchimba na kufua 'madini' hayo.

Hata klabu za Tanzania Bara ambazo zinacheza Ligi Kuu na ngazi za chini, zinaonekana kama kuichukulia poa Zanzibar, lakini ni sehemu ambayo zinaweza kupata wachezaji wazuri kwa gharama nafuu, kwani wanachokosa huko ni lishe bora anayopaswa kupata mchezaji, mafunzo ya kupambana kusaka ushindi na pia kutofautisha kucheza rafu na kutumia nguvu.

Wachezaji wengi wa Zanzibar wanaonekana kucheza zaidi rafu ni kwa sababu tu, wanajua kuwa wana udhaifu kwenye kutumia nguvu. Watakapopata mafunzo sawasawa ya namna gani ya kutumia nguvu, ukijumlisha na ufundi walionao, watakuwa na soko kubwa mno Tanzania Bara.

HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mauzo wa Airtel Tanzania Mkoa wa Rukwa, Bartholomew Masatu (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga, Sebastian Waryuba, baadhi ya msaada wa chakula uliotolewa na kampuni ya Airtel kwa kituo cha watoto yatima cha Katandala mjini Sumbawanga. Kulia ni mkuu wa kituo hicho, Lucy Maganga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa awahimiza wasimamizi miradi maendeleo kwenda kasi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka viongozi na watendaji wanaosimamia miradi ya ujenzi kuongeza kasi ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na kuwapa fursa wananchi wafaidi matunda ya mapinduzi matukufu ya Zanzibar.

Alitoa wito huo jana, wakati akizungumza na mamia ya wakazi wa Jimbo la Kiwani, Mkoa wa Kusini Pemba baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo cha afya cha shehia ya Kendwa ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za sherehe ya miaka 58 ya Mapinduzi Zanzibar.

"Nitumie fursa hii kuwaomba viongozi na watendaji wanaosimamia mradi huu waendelee kushirikiana na kufanya kazi kwa kasi zaidi ili kukamilisha ujenzi huu kwa wakati uliopangwa ili kuwapa fursa wananchi wafaidi matunda ya mapinduzi matukufu ya Zanzibar."

Pia amewataka viongozi wa shehia hiyo washirikiane na Wizara ya Afya kuhakikisha majengo na miundombinu iliyowekwa inatunzwa vyema ikiwamo vifaa vitakavyonunuliwa sasa kwa matumizi ya sasa na baadaye.

Aliwataka watumishi watakaopangiwa kuishi kwenye nyumba ya daktari wa kituo hicho, wayatunze majengo hayo, kupanda miti na kutunza mazingira yanayowazunguka.

Akizungumzia uboreshaji wa huduma za afya, Waziri Mkuu alisema lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kujenga vituo vingi zaidi ili wananchi wasiende umbali mrefu kutafuta huduma hizo.

"Ninawasihi tuiunge mkono nia njema iliyoonyeshwa na Mheshimiwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi."

Waziri Mkuu ambaye kabla ya kuweka jiwe la msingi alikagua majengo matatu ya kituo hicho, alisema ameridhishwa na ujenzi wake na hasa kiwango cha ubora kilichoko.

"Nilipofika, nimekagua majengo kuanzia chini hadi juu. "Naipongeza kamati ya usimamizi wa ujenzi wa kituo hiki kwa kusimamia vizuri ujenzi wa kituo hiki. Ninaziagiza kamati nyingine hapa nchini, ziige mfano wa Kamati hii ya Kendwa. Niliposikia fedha iliyotumika sikuamini. Fedha kidogo, lakini imetoa majengo mazuri yenye viwango."

Mapema, akitoa taarifa ya ujenzi wa kituo hicho, Msimamizi Mkuu wa Majengo kutoka ZBA, Mhandisi Said Malik Said, alisema ujenzi wa kituo hicho unaofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), ulianza Agosti 28, mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Februari 27, mwaka huu.

"Gharama za ujenzi ni Sh. milioni 388, lakini hadi sasa zimetumika Sh. milioni 270. Kitakapokamilika, kituo kitakuwa na majengo ya OPD, maabara, chumba cha daktari, vyoo, chumba cha kumfanyia mgonjwa uchunguzi wa awali, chumba cha sindano na kufunga vidonda, kitengo cha meno, wodi ya kinamama wajawazito na nyumba ya daktari yenye uwezo wa kuchukua watumishi wawili kwa pamoja (2-in-1).

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema kutokana na mabadiliko ya sheria, ujenzi wa kituo kama hicho utaendelea kwenye shehia zote.

Alisema kutokana na uhakiki wa walengwa wote uliofanyika Julai 2020 hadi Januari 2021, kaya 1,992 zilisema zinaishukuru serikali na kwa hiari yao, zikaamua kujitoa rasmi kwenye mpango wa TASAF wa kuhudumia kaya maskini.

"Kupitia uhakiki huo, kaya nyingine 211,800 zimekiri kuondokana na hali duni, na kwa hiyo, wako tayari kujitoa kwenye mpango huo baada ya miezi sita. Kutokana na uimarishaji lishe, afya na elimu, uandikishaji shuleni umeongezeka na mahudhurio pia yameongezeka."

Alisema watoto wengi waliosaidiwa na mpango huo, walipata matokeo mazuri ya ufaulu wa daraja la kwanza hadi la tatu. "Matokeo yake, watoto 782 waliohitimu mwaka jana, wamechaguliwa kwenda vyuo vikuu mbalimbali hapa nchini. Na hawa wamesaidiwa kupata ufadhili wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu," alisema.

Akielezea mafanikio mengine ya mradi huo, Mwamanga alisema waliwahimiza walengwa wa mradi huo kote nchini wawe wanatunza akiba kutokana na miradi wanayojishughulisha nayo. "Matokeo yake, vikundi 23,000 kutoka maeneo 71, vyenye wanachama zaidi ya 350,000 vimejiwekea akiba ya Sh. bilioni 6.9 na miongoni mwao, vimekopeshana Sh. bilioni 2.6 ili waweze kushiriki shughuli za kiuchumi."

Hafla hiyo ya uwekaji jiwe la msingi ilihudhuriwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee na Watoto, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Wilaya za Mkoani, Chakechake, Wete na Micheweni, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na viongozi wengine mbalimbali.

# TANROADS, TARURA waombwa kuongeza barabara

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), wameombwa kuangalia uwezekano wa barabara inayojengwa kutoka Handeni- Kilindi mkoani Tanga hadi Kijiji cha Makiungu, mkoani Singida, kuifikisha kwenye kata tatu kuongeza wigo wa usafiri mkoani humo.

Wametaka ifike kijiji cha Minyinga, kata za Unyamikumbi, Mungumaji, Misuna hadi Majengo, Manispaa ya Singida.

Ombi hilo lilitolewa na madiwani wa kata hizo wakati wa mkutano maalumu wa Baraza la Madiwani Halmashauri ya Singida, kujadili rasimu ya mpango wa bajeti na matengenezo na ujenzi wa barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Singida.

Diwani wa Kata ya Mtamaa, Gwae Mbua, alisema mji wa Singida unakua kwa kasi na mahitaji yake ni makubwa, ni wakati muafaka kwa serikali kuongeza bajeti, kwa kuwa mkoa huo ni sebule ya makao makuu ya nchi.

Gwae ambaye amewahi kuwa Meya wa Manispaa ya Singida, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa zaidi ya Sh. bilioni 2.2 za miradi mbalimbali.

Akiwasilisha taarifa ya rasimu ya mpango wa bajeti na matengenezo na ujenzi wa barabara za Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Singida, Mhandisi Christopher Njalika, alibainisha kuwa TARURA inatarajia kutumia Sh. 2,284,671,658.09 kukarabati na kutengeneza barabara zenye urefu wa kilomita 116.4 na makalavati 95 katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha wa 2022/2023 hadi 2025/2026. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022 Wakala ulitengewa Sh. 1,284,671,658.09 kwa ajili ya ukarabati wa barabara, vile vile ulipokea Sh. 1,000,000,000 za maendeleo ikiwa ni ziada ya bajeti kutoka katika tozo ya mafuta na fedha za mfuko wa jimbo.

Mhandisi Njalika, alibainisha kuwa mwaka huu wa fedha TARURA, ilipokea Sh. 2,284,671,658.09 kwa ajili ya shughuli za ukarabati na ujenzi wa barabara za Manispaa ya Singida.

"Wakala umeandaa mpango wa ukarabati na matengenezo ya barabara wa miaka minne kuanzia mwaka wa fedha wa 2022/2023 hadi 2025/2026 kufuatana na ukomo wa fedha, mwaka huu tunaoendelea kuutekeleza wa 2021/2022 wenye jumla ya Sh. 2,284,671,658.09," alisisitiza.

Alisema katika mpango huo, wanategemea kutekeleza ujenzi wa barabara za lami zenye jumla ya kilomita 2.4, barabara za changarawe kilomita 107, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa kilomita saba na makalavati 95.

Kwa mujibu wa mhandisi huyo mpango huo unazingatia ukubwa wa barabara, wingi wa watumia barabara, uwapo wa taasisi, matatizo na kero kwa wananchi na kwamba barabara zilizoainishwa fedha za Benki ya Dunia zimeachwa ili kuondoa mgongano endapo vyanzo hivyo vitatoa fedha kwa matengenezo hayo.

Akifunga mkutano huo, Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Maulidi Kyaratu, aliwashukuru madiwani kwa umoja wao wa kupitisha rasimu hiyo ya mpango wa bajeti.

Alisema TARURA haina budi kuwashirikisha madiwani kwa uhakika kwenye maeneo ambayo mradi huo unapita na haitakuwa vyema wakati mradi unapoendelea kutekelezwa, diwani husika awe kama mtazamaji wa kawaida.

# Kunenge ataka wazazi kuweka kipaumbele elimu

**Na Julieth Mkireri**, KIBITI

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema endapo wazazi wataweka kipaumbele cha elimu kwenye jamii zao watapunguza mzigo kwenye familia na kuwa na maendeleo kwenye maeneo yao.

Kunenge aliyasema hayo jana alipokuwa akikagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Halmashauri ya Kibiti vilivyojengwa kwa fedha za Maendeleo ya miradi kwa ustawi wa taifa.

Alisema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na wazazi wanatakiwa kusimamia suala la watoto wao kusoma na kufaulu ili waweze kuwa na maendeleo.

Kunenge alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa umeondoa kero ya awali ya mrundikano wa wanafunzi katika chumba kimoja pamoja na kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu na kwamba juhudi zinatakiwa kuelekezwa kuwasimamia wanafunzi kwenda shule.

"Mzazi ambaye atabainika hajampeleka shule mtoto anayestahili kuanza masomo hatua za kisheria zitachukuliwa kwani atakuwa anamnyima haki yake ya kupata elimu ndiyo sheria inavyosema na utaratibu.

"Hili nalisema nikiwa kama kamisaa kila kiongozi ahakikishe watoto wanaenda shule na nitakapobaini kuna eneo watoto hawaendi shule, viongozi wa eneo husika wachukuliwe hatua hawatoshi kwa maana watakuwa wanamhujumu Rais ambaye anapambana watoto wapate sehemu nzuri ya kupata elimu," alisisitiza.

Mkuu huyo wa mkoa ambaye aliambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa, aliwataka watoto wa kiume kuacha tabia ya kukatisha masomo na kufanya biashara ndogo ndogo ikiwamo kuchunga mifugo.

"Kinamama niwaombe msimamie watoto wa kike wasome ndoa zitakuja baadaye, kumbukeni mkiwasomesha watakuwa sio mizigo kwenu, napennda nione watoto wa kike wanasoma," alisema.

Kunenge alisema kazi aliyoifanya Rais Samia Suluhu ni kupata fedha na kujenga vyumba katika maeneo yote ambayo yalikuwa na vikwazo na kuwawezesha wanafunzi wote wa kidato cha kwanza wanapata nafasi. Mkoa huo ulipatiwa Sh. bilioni 13.3 na kati ya hizo sh. bilioni 10 zimetumika kujenga miundombinu ya elimu vyumba 422 kwa shule za sekondari ambavyo vimekamilika kwa asilimia 100 na vyumba 133 kwa shue shikizi na fedha zilizosalia ni kwa ajili ya miundombinu ya afya.

Kwa mujibu wa Kunenge wanafunzi wanaotarajiwa kuanza masomo kwa madarasa ya awali ni 30,479 hadi sasa ni asilimia 41.6 pekee ambao wameandikishwa huku kwa upande wa darasa la kwanza wanaolengwa kuandikishwa ni 52,709 na asilimia 51.44 ndiyo wameandikishwa.

Alisisitiza uandikishaji ufanyike kwa haraka kwa kuwa endapo malengo yatafikiwa itakuwa ni zawadi kwa Rais ambaye ameamua kupambana na kero za elimu kwa upande wa miundombinu.

Hamza Bakari, mmoja wa wakazi wa Kibiti alisema ujenzi wa vyumba kwenye shule shikizi umeondoa kero ya wanafunzi kutembea umbali mrefu.

Alisema baadhi ya wanafunzi walikuwa wakikatisha masomo kutokana na umbali wa shule na watoto wa darasa la awali walikuwa wakilazimika kuanza wakiwa na miaka mitano hadi saba.

"Tunampongeza Rais wetu kwa kututatulia kero ya msongamano wa wanafunzi kwenye vyumba, lakini pia kuondoa kikwazo cha wanafunzi kukatisha masomo kutokana na umbali wa shule, kwetu wazazi tumefarijika na tutahakikisha watoto wetu wanaenda shule," alisema.

Katika ziara hiyo aliwapongeza wakuu wa wilaya, Wakurugenzi na wananchi kwa ushirikiano walioonyesha katika kukamilisha miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na kukamisha kwa wakati.



Meneja wa Benki ya NMB tawi la Madaraka jijini Tanga, Elizabeth Chawinga, akimkabidhi Ofisa Uhusiano wa Wateja wa benki hiyo, Godfray Methew, kuzungumzia huduma za bima zinazotolewa na benki kwenye kongamano la elimu lililofanyika jijini Tanga, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chamwino yatengewa bil. 3/- madarasa

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 2.92 za mradi wa UVIKO-19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 146 katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino jijini Dodoma.

Wananchi hao wa halmashauri pia wametakiwa kuwahamasisha watoto wao kusoma katika madarasa hayo yaliyojengwa kwa mradi wa UVIKO-19, ili yalete tija.

Akizungumza mwishoni mwa wiki jijini hapa katika ziara ya kutembelea Wilaya ya Chamwino kuona madarasa hayo, Mkuu Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema moja ya halmashauri iliyopata fedha nyingi kwa madarasa ni Wilaya ya Chamwino na kwamba inapaswa kuonyesha bidii katika ujenzi unaoendelea.

Alisema wilaya hiyo imewekewa bajeti kubwa katika mradi wa madarasa nao wanapaswa kuonyesha jitihada za kuyatunza. "Nampongeza Rais wetu Samia Suluhu Hassan pamoja na serikali yake kwa ujenzi huu pia naishukuru kwa kutupatia halmashauri yetu Sh. bilioni 2.92 hili ni jambo la kujivunia," alisema Mtaka.

Aliwapongeza wananchi wa wilaya hiyo kwa kuwa walinzi wa vifaa vya ujenzi pamoja na miundombinu.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, alisema Chamwino imepewa upendeleo mkubwa katika fedha hizo, hawawezi kumwangusha Rais ndiyo maana ujenzi umekamilika kwa wakati.

Alisema anampongeza Rais Samia kwa kuweka kipaumbele katika suala la elimu na wasaidizi wake hawatamwangusha.

Aliwasisitiza wakazi wa eneo hilo kuhakikisha wanawaleta wanafunzi watakaochaguliwa kujiunga na shule hiyo ya sekondari.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Msanga, Hatibu Luwumba, alisema shule hiyo imepewa Sh. milioni 60 na wananchi walichangia Sh. milioni 1.6. Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma (CCM), Godwin Mkanwa, alisema mafundi wanaojenga madarasa kupitia mradi wa UVIKO-19 wamejengewa uwezo na serikali.

"Nawapongeza wananchi na viongozi wa wilaya hii katika kujitolea kuchangia ujenzi wa madarasa," alisema.

Akizindua madarasa hayo, Mtaka aliipongeza serikali kwa mradi huo

na kuwataka wananchi wahakikishe hakuna mtoto anayebaki nyumbani bila kusoma.

## Mwekezaji aomba serikali kutoa ardhi viwanda kuchakata mpunga

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MWEKEZAJI wa kiwanda cha kuchakata mpunga Mbarali, mkoani Mbeya na Makambako, mkoani Njombe, Venance Mgeni, ameiomba serikali kuwapatia ardhi wawekezaji wenye viwanda ili waweze kuzalisha zao hilo kama sehemu ya malighafi muhimu katika uendeshaji wa viwanda hivyo.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, Mgeni ambaye ni mwekezaji wa viwanda vya Nass Digital Rice Mill, alisema kumekuwapo na jitihada kubwa za serikali hasa ya awamu ya tano kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda nchini.

Alisema kupitia uhamasishaji huo Watanzania wazawa walilazimika kuanzisha viwanda vya uchakataji wa zao la mpunga katika eneo la Mbarali ambalo linazalisha kilimo cha mpunga kwa wingi na Makambako mkoani Njombe ili kuwezesha wakulima kuongeza thamani ya mazao yao kwa kutumia mashine za kisasa katika uchakataji wa zao hilo.

Alisema, iwapo serikali kupitia wizara husika ya Uwekezaji, Kilimo pamoja na Wizara ya Ardhi zikaweka mkakati wa pamoja na kuwezesha wawekezaji wa viwanda vya kuchakata mpunga kuwa na ardhi ya uzalishaji wa zao hilo, itasaidia viwanda hivyo kuwa endelevu badala ya kusubiri msimu wa mavuno ili wakulima walete mpunga wao.

Alisema inawezekana viwanda hivyo kuwa na mashamba ya uzalishaji iwapo watawezeshwa kupata ardhi kupitia mashamba hayo watakuwa na kazi endelevu ya uchakataji mpunga kupitia mazao wanayolima na yale ya wananchi.

Pia alisema kwa sasa kiwanda cha Makambako pekee kimeweza kutoa ajira kwa vijana zaidi ya 70 ambao wanaendelea na kazi ya uchakataji mpunga baada ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) kuwapatia kazi ya kukoboa mpunga.

Alisema pamoja na kuwapo kwa mafanikio makubwa, bado zipo changamoto za tozo na kodi ambazo zinawabana wawekezaji na kuomba serikali kuangalia sekta hiyo ya viwanda ambayo ni nguzo kubwa ya ajira na suala la tozo na kodi linapaswa kuangaliwa zaidi.

## HABARI KITAIFA

# Tunduma yatumia bil. 1.5/- mapato ya ndani ujenzi miradi ya maendeleo

**Na Thobias Mwanakatwe**

HALMASHAURI ya Mji wa Tunduma, Wilaya ya Momba, mkoani Songwe, imetumia Sh. 1,507,936,715.62 ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Philemon Magesa, aliwaeleza wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Momba wakiongozwa na Mwenyekiti wa chama hicho, Twaha Maulid, waliofanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na halmashauri hiyo. Magesa alisema fedha zinazotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo ni za makusanyo ya ndani kwa mwaka wa fedha wa 2020 hadi 2021 na halmashauri hiyo ilikusanya Shilingi bilioni tano.

Akifafanua kuhusu miradi hiyo mbele ya wajumbe hao wa Kamati ya Siasa ya wilaya, Kaimu Mhandisi wa halmashauri hiyo, Mhandisi Dickson Kisenime, alisema fedha hizo zimegawanywa katika miradi mitatu. Aliitaja miradi hiyo na gharama zake kuwa ni wa ujenzi na ukarabati wa maeneo ya wafanyabiashara wadogo (masoko) katika mitaa ya Majengo, Maporomoko, Stend Kuu na Tazara unaogharimu Sh. 451,808,211.62.

Mradi mwingine ni ujenzi wa kituo cha afya cha Kata ya Chwapwa, ambacho gharama yake ni zaidi ya Sh. milioni 400, pamoja na mradi wa ujenzi wa shule mpya ya msingi Haisoja iliyopo kata ya Sogea, utakaogharimu Sh. 656,128,04.2. Kwa upande wake, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Momba, Mauld alimshukuru Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo na timu yake kwa kutekeleza miradi ya maendeleo katika halmashauri hiyo ya Mji Tunduma.

Alisema kamati yake imeridhishwa na miradi yote waliyoitembelea na kuikagua ambayo italeta tija kwa maendeleo ya wananchi wa Tunduma na Wilaya ya Momba.



Mratibu wa kamati ya viongozi wa dini mbalimbali nchini, Edmund Matotay, akizungumza wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliofanyika mwisho wa wiki jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# W'biashara waonywa kupulizia dawa nyama

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WAFANYABIASHARA wa nyama mkoani Katavi, wametakiwa kufuata sheria na taratibu za uuzaji wa nyama, ikiwamo kutopuliza dawa zenye sumu za kuua wadudu ili kuepusha madhara kwa walaji.

Akizungumza na wafanyabiashara hao jana, Ofisa Mifugo Mkoa wa Katavi, Zediel Muhando, alisema kwenye biashara hiyo watabaki na watu wachache watakaokidhi vigezo japokuwa sio lengo lao na wanafuatilia kwa karibu wanaonyunyuzia dawa kwenye nyama kudhibiti wadudu bila kuzingatia utaratibu.

"Unakula sumu hupati madhara leo, lakini baadaye yanakuja kuathiri kizazi na kizazi, utaambiwa una saratani ya ini, ini limeharibika sababu yanapokea sumu nyingi maana unakula nyama imepuliziwa sumu, nyanya imepuliziwa sumu, mahindi pia yamepuliziwa sumu hii siyo sawa kabisa," alibainisha Zediel.

Kwa upande wake, Ofisa Mkaguzi Bodi ya Mifugo Kanda ya Magharibi, Kulwa Joseph, alisema lengo la ukaguzi huo ni kusimamia ubora kwa kuhakikisha uzalishaji wa nyama kutoka kwa mfugaji hadi mlaji ni salama kwa afya.

Alisema vitu wanavyo zingatia wanapofanya ukaguzi kwenye mabucha na machinjio ni usafi sehemu zote mbili, wauzaji kupima afya zao, ubora wa majengo wanayofanyia biashara, mavazi stahiki kwa muuzaji na kuzuia matumizi ya magogo.

"Nilikuwa napitapita kwenye machinjio haya nikaona kuna mto kule chini cha ajabu kuna mtu alikuwa anaosha nyama pale kwenye ule mto, pembeni kuna mama naye anaosha mboga, baadaye wanatuletea tuje kula yale maji hatujui yanatiririka kutoka wapi, yana kemikali gani huko yalikotoka, lakini hata ukiyaangalia tu kiafya hayana ushirikiano," alibainisha Kulwa.

Kwa mujibu wa Kulwa, wamemwelekeza mwakilishi wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda kuhakikisha machinjio inakuwa na uzio ili kuzuia mwingiliano wa wanyama holela wakiwamo fisi na wanyama wengine.

# Wapendekeza hospitali kuitwa Samia

**Na Abdallah Khamis, MTWARA**

KIKAO cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mtwara (RCC), kimeibuka na maazimio saba ikiwamo kupendekeza jina la Hospitali ya Rufani Kanda ya Kusini kuitwa 'Samia Zone Referral Hospital Mikindani Mtwara'.

Pia kikao hicho kilichokaa mwishoni mwa wiki chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Brigedia Jenerali Marco Gaguti, kwenye elimu kiliazimia kujenga mabweni kwa shule za sekondari kwa kila halmashauri.

Kuimarisha vivutio vya mahudhurio shuleni kwa kuendesha michezo na bendi, kutoa chakula, viongozi wa kisiasa na viongozi wa dini kushiriki kikamilifu kuhamasisha jamii ya wana-Mtwara umuhimu wa elimu, pamoja na mpango kazi wa elimu wa mkoa wa kutaka asilimia 98 ya wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza waweze kufika kidato cha nne utekelezwe ipasavyo.

Kwenye elimu, waliazimia kutoa motisha na mafunzo ya kiutendaji kwa walimu kazini, pamoja na uongozi wa mkoa kukaa na uongozi wa mfuko wa elimu na kuangalia halmashauri zitakavyochangia utoaji wa motisha kwa walimu na wanafunzi watakaofanya vizuri.

Kikao kilikataa taarifa ya mamlaka ya maji mkoa kutokana na kutokuwa na takwimu sahihi ya hali ya upatikanaji wa huduma hiyo.

Katika eneo hilo kikao hicho kilikubaliana kuundwa kamati ya utafiti na kuja na taarifa sahihi ya upatikanaji wa maji kwenye mkoa mjini na vijijini kusaidia vikao vijavyo kufanya uamuzi wakiwa na uelewa wa pamoja.

Kiliazimia pia kuwapo kwa maboresho katika mifumo ya upimaji wa mafuta katika Bandari ya Mtwara kwa ajili ya kupunguza gharama za kiutendaji na kutoa nafuu ya nishati hiyo kwa wakazi wa mikoa ya kusini wanaotumia bandari hiyo.

Eneo la kilimo, RCC ilikubaliana kuhuisha zao la korosho kwa lengo la kufikia uzalishaji wa tani 406,000 ifikapo mwaka 2025, na mazao mengine kwa ajili ya kuchangia uchumi wa mkoa huo.

Katika eneo hilo kikao kilielezwa kuwa mkoa una mazao mengine zaidi ya 20 yanayofaa kibiashara, lakini hayapewi uzito unaostahili kama ilivyo korosho.

Pia waliazimia na kuitaka Bodi ya Korosho, kutafuta masoko ya uhakika na yenye tija na bei ya kuridhisha kwa ajili ya kuwasaidia wakulima.

Kwenye upande wa umeme kiliazimia Shirika la Umeme Mkoa wa Mtwara (TANESCO), kusimamia mpango kazi wa umeme vijijini, awamu ya tatu mzunguko wa pili kwa ajili ya kuleta ufanisi wa upatikanaji wa huduma hiyo vijijini na mpango kazi wao uwasilishwe kwenye ngazi zote za mkoa kwa ajili ya kufuatilia ufanisi.

Kuhusu mikopo ya asilimia 10 inayowalenga vijana wanawake na wenye ulemavu, kikao hicho kiliazimia itekelezwe kwa mfumo asilimia 60 kuelekezwa katika miradi mikubwa yenye tija itakayozalisha ajira ya jumla jumla na asilimia 40 zibaki katika utaratibu wa kawaida wa kuwawezesha wananchi kiuchumi, ikiwamo nafasi ya mgawanyo wa asilimia 10 ya vijana wazee na wenye ulemavu itakayotoka katika mapato ya halmashauri.

Awali katika majadiliano hayo, Mbunge wa Newala, George Mkuchika, alitaka kikao kiazimie suala la kubinafsishwa kwa viwanda vya kubangua korosho ambavyo kwa sasa havifanyi kazi ili wawekezaji wavihuishe na kuleta tija kwa wakulima.

Alisema ni wakati muafaka kwa msajili wa hazina kutoa mwelekeo wa kubinafsisha viwanda vya kubangua korosho Mkoa wa Mtwara, hata hivyo, Mbunge wa Masasi Geofrey Mwambe alisema suala la ubinafsishaji wa viwanda linashughulikiwa na kwa sasa kuna mgogoro wa kisheria unaosubiri kutatuliwa.

Katika hatua nyingine kamati ya amani mkoa wa Mtwara wakichangia hoja katika kikao hicho, walieleza kuwa wameridhishwa na namna wanavyoshirikishwa katika matukio mbalimbali ya kimaendeleo ndani ya mkoa huo kupitia kwa Mkuu wa Mkoa.

# H'shauri yakopesha vijana pikipiki za mil. 26/-

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI Manispaa ya Morogoro imekabidhi pikipiki 10 zenye thamani ya Sh. milioni 25.8 kwa kikundi cha Bomsate cha Kata ya Mafisa kinachojishughulisha na usafirishaji abiria kituo cha mabasi Msamvu ikiwa ni hatua ya kuwawezesha vijana kiuchumi.

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa ya Morogoro, Rutahiwa John, alikabidhi pikipiki hizo zilizotolewa mkopo jana kwa Mwenyekiti wa kikundi hicho, Awadhi Hamis. Alisema pikipiki hizo ni sehemu ya uwezeshwaji unatokana na fedha za makusanyo ya ndani ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali la kutenga asilimia 10 ya bajeti ya halmashauri kila mwaka kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Tumeelekezwa na Rais Samia Suluhu Hassan fedha hizi ambazo wanapewa makundi haya zitolewe bila riba ili kila mmoja awe mnufaika wa kujikwamua kiuchumi," alisema Rutahiwa.

Aliwashauri wanaopata mikopo hiyo kuzingatia vigezo na masharti ya kurejesha kwa wakati ili na wengine waweze kunufaika na fursa kwa ajili ya maendeleo yao.

Rutahiwa alisema, Manispaa ya Morogoro itaendelea kuhamasisha wananchi wake uwapo wa asilimia 10 kwa ajili ya kuwawezesha na kuwainua kiuchumi ikizingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Awadhi Hamis, alisema baada ya kupewa pikipiki 10 za mkopo, kwa sasa kina jumla ya pikipiki 30.

"Pikipiki hizi zimekuja kutokana na kazi nzuri tunazozifanya na kurejesha mkopo kwa wakati, safari hii tumekopeshwa pikipiki 10 na kufanya jumla kuwa 30, mkopo tulioupata tutahakikisha tunautumia vizuri na kufanya marejesho kwa wakati," alisema Hamis.

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa White House, Kata ya Mafisa, Said Yassin ambako kikundi hicho ni eneo lake la utawala (kiliposajiliwa), aliupongeza uongozi wa Manispaa ya Morogoro kwa kuona umuhimu wa kusaidia jamii hasa vijana katika kuwainua kiuchumi.




Washindi wa promosheni ya "Show Love, Tule Shangwe" ya Vodacom Tanzania wakiwa na zawadi baada ya kukabidhiwa na Meneja Mkakati wa Biashara wa kampuni hiyo, Magreth Lawrence (watatu kulia), kwenye hafla iliyofanyika jijini Mbeya, jana. Katikati ni mwendesha promosheni hiyo Masta Shangwe. Msimu huu wa sikukuu Vodacom inatoa zawadi kwa wapendanao ambapo wateja wanaweza kununua bando na kutumia huduma ya M-Pesa kwa kupiga *149*01#. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majukwaa yasaidia wanawake kuondoa woga kukopa

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

UANZISHAJI wa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, umewasaidia kuondoa woga wa kuingia katika taasisi za kifedha kuomba mikopo kwa kuogopa askari wanaolinda maeneo hayo.

Awali, walikuwa waoga kuingia kwenye benki kutafuta fursa za mikopo kwa madai ya kuogopa askari wanaolinda taasisi hizo na kukosa fursa za mikopo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Robert Kwela, alisema hayo jana wakati wa ufunguzi wa uzinduzi wa jukwaa la uwezeshaji wanawake kiuchumi na kusema muda umefika kwa kundi hilo kubadilika na kujiingiza katika masuala ya kukuza uchumi wao.

Alisema, wanawake wengi wanaoishi katika maeneo ya pembezoni ni waathirika katika kujenga urafiki na taasisi za kifedha na kwamba kuundwa kwa majukwaa hayo kutakuwa suluhisho la kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kutoka ngazi za mitaa, vijiji, kata, wilaya hadi taifa.

Kwela alisema, halmashauri hiyo imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuwakopesha mikopo isiyokuwa na riba wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye ulemavu ili kuhakikisha wanakuwa kimitaji na kwamba fursa nyingine za mikopo zinapatikana katika taasisi za kifedha.

"Mwaka huu wa fedha 2021/2022 tumetenga Sh. milioni 637 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, hivyo changamkieni fursa hii ili mkuze biashara zetu kwa kutanua wingi wa mitaji," alisema Kwela.

Alisema, jukwaa hilo litasaidia kwa kiasi kikubwa kuwaunganisha wanawake wajasiriamali kupitia semina, makongamano mbalimbali na kupata fursa ya kufanya majadiliano yatakayo wasaidia kukuza masoko ya biashara zao na mitaji waliyo nayo.

Akitoa taarifa ya uzinduzi wa jukwaa hilo, Hilda Robert alisema, kumekuwa na ubaguzi mkubwa wa kiuchumi baina ya makundi ya wanawake na wanaume na kusahau kuwa mwanamke ni kichocheo cha maendeleo nchini na kupewa kipaumbele cha mikopo kundi la wanaume.

Alisema, tayari majukwaa 97 yameanzishwa, kati ya hayo 35 yapo ngazi ya mitaa, 42 vijiji, 20 kata na lengo la uanzishwaji ni kuhakikisha wanawakutanisha wajasiriamali wote na wanajadili na kutatua changamoto zinazowakabili.

Naye Mkuu wa Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Kanda ya Ziwa, Jozaka Bukoku, alisema, uanzishwaji wa majukwaa hayo ni mwongozo kutoka katika Baraza la Uwezeshaji la Taifa na wanajihusisha pia na kutoa programu za wanawake kwa wingi na hivi karibuni watawapatia elimu mama lishe.

Katibu Tawala Wilaya ya Kahama, Timoth Ndanya, alisema, wanawake ni jeshi kubwa na kuwataka kutumia jukwaa hilo kubadilishana uzoefu na watu kutoka taasisi mbalimbali ili kurahisisha mafanikio yao.

Alimtaka, ofisa huyo kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba majukwaa hayo ili kutatua changamoto ya ukosefu wa mitaji na kuondokana na dhana ya kuwa tegemezi kwenye familia na jamii wanazotoka.

# Imani potofu yazorotesha watu kuchanja

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, amesema bado jamii inakabiliwa na changamoto ya imani potofu kuhusu chanjo ya UVIKO-19 kwamba inasababisha magonjwa, na nguvu za kiume kupungua.

Sendiga aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo yaliyoandaliwa na Wizara ya Afya kupitia mpango wa taifa wa chanjo kwa waandishi wa habari kutoka mikoa ya Njombe na Iringa.

Alisema kuwa jamii inapaswa kupewa elimu ya kuhakikishiwa kwamba chanjo ni salama kwa afya zao.

"Imeelezewa hapa kwamba kama nchi jitihada za kuhakikisha wananchi wanapata chanjo ya UVIKO-19 zimekuwa kubwa, lakini kama nchi tumekuwa tukifahamu tunayo magonjwa mbalimbali ya mlipuko, lakini tuna chanjo kadha wa kadha kwa ajili ya watoto wadogo wa umri tofauti na watu wazima pia," alisema Sendiga.

"Sasa jitihada kubwa zimekuwa kwenye UVIKO-19 ambayo tunategemea na nyie muende kuifanya, lakini sambamba na hiyo tutakwenda kusaidiana kupeleka elimu katika chanjo nyingine ambazo zinaendelea kutolewa kwa watoto wale wa chini ya miaka mitano ambao tunafahamu kwamba nao ni lazima wapate chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali mtaalamu ameeleza hapa kuna magonjwa ya surua kwa watoto ambayo nayo yanatolewa chanjo sasa tumekazana kwenye suala moja," alisema.

Alisema kuna magonjwa ya polio, kifua kikuu, pepopunda na mengine ambayo chanjo lazima zisisitizwe, zitolewe elimu, zielezwe kwa undani na kwa umakini ili wananchi wa rika tofauti waweze kukumbuka.

Sendiga alisema lengo la kuanzisha chanjo dhidi ya magonjwa mbalimbali ya mlipuko ni kuikinga jamii na athari mbalimbali ikiwamo ulemavu wa kudumu pamoja na vifo.

Awali, ofisa programu mpango wa taifa wa chanjo, Lotalis Gadau, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwakumbusha waandishi wa habari kuendelea kutoa elimu ya chanjo UVIKO-19 na afua nyingine za chanjo ili kwenda pamoja.

"Pamoja na kuendelea kuelimisha watu kuchanja, lakini tusisahau afua nyingine za chanjo ili mwisho wa siku tusijikute tunashinda kwenye UVIKO-19, tukaanza kupata milipuko ya surua," alisema Gadau.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WAKUTAZAMWA ZAIDI FAINALI ZA AFCON 2022 UK. 12 - 13



XHAKA & AUBAMEYANG

# NYOTA WATANO WALIOSHTUKIZWA KWA KUVULIWA UNAHODHA

**LONDON,** Uingereza

KUWA nahodha wa klabu kunakuja na majukumu mengi. Si tu kwamba, unapaswa kuongoza kwa mfano na kuwa mfano wa kuigwa kwa wenzako, lakini unahitaji kuwa muwazi. Klabu zilizofanikiwa zimekuwa na haiba kubwa na kiongozi anayefaa.

Chukua, kwa mfano, Manchester United iliyoshinda mataji matatu mwaka 1999. Roy Keane ni mtu ambaye ungependa kuandamana naye kwenye vita.

Au Patrick Vieira wa Arsenal 'Isiyofungika' na Steven Gerrard wa Liverpool ni nahodha mwingine maarufu.

Wakati wote mambo yanapokuwa shawri nahodha huwa na wakati mzuri wa kuota utukufu. Lakini hali inapokuwa ngumu, wao ndio wa kwanza kuchunguzwa. Kwa kuzingatia matukio ya hivi majuzi, hapa tunawaangalia manahodha watano waliovuliwa unahodha, twende sasa...

### #5. JOEY BARTON (QUEENS PARK RANGERS)

Joey Barton si mgeni kwa matatizo ya kinidhamu. Alikuwa mkorofi ndani ya dimba na mara nyingi huongeza masuala kwa urefu usio wa lazima. Ushindi wa 3-2 wa Manchester City dhidi ya Queens Park Rangers siku ya mwisho ya msimu wa 2011-12 uliwafanya wabebe taji la Ligi Kuu.

Kile ambacho mara nyingi husahaulika au kufunikwa na uwezo wa Sergio Aguero kwa kufunga bao dakika za mwisho ni uhalifu wa Barton katika mchezo huo huo.

Inafaa kukumbuka kuwa Barton alichezea City kati ya mwaka 2002 na 2007, lakini hakutaka sana ustaarabu.

QPR ilihitaji angalau sare moja au Bolton Wanderers kupoteza mchezo wao siku ya mwisho ya msimu ili kubakia Ligi Kuu. Hata hivyo, nahodha wao alikuwa Barton na alimpiga kiwiko cha usoni mchezaji mwenzake wa zamani, Carlos Tevez. Hakuishia hapo akampiga teke Aguero nyuma ya goti lake baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu.

Pia alijaribu kumpiga kichwa Vincent Kompany na kutaka kupigana na Mario Balotelli kabla ya kuvutwa na Micah Richards. Barton aliteseka kwa haki baada ya matokeo. Alivuliwa unahodha na akatolewa kwa mkopo kwenda Marseille.

### #4. MAURO ICARDI (INTER MILAN)

Kwa muda ilionekana kama Mauro Icardi alikuwa na jambo zuri likiendelea Inter Milan. Alikuwa mmoja wa manahodha wachanga zaidi katika historia ya klabu hiyo na alikuwa akifunga mabao mengi. The Nerazzurri ilionekana kuwa sawa na mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina ambaye alikuwa na utata.

Hata hivyo, aliwachambua wachezaji wa Inter kwa kuwarushia shutuma nyingi kwenye kitabu chake. Mkewe Wanda Nara kisha alizungumza kuhusu wachezaji na usimamizi wa Inter Milan katika onyesho lililoitwa Tiki-Taka. Hilo liliishia kuvuliwa unahodha kwa Icardi.

Klabu haikumruhusu nahodha na mkewe kudhoofisha taasisi hiyo. Mara moja akavuliwa unahodha. Je, Icardi aliipokea vizuri? Hapana. Alikataa kuichezea Inter Milan katika mechi ya Ligi ya Europa dhidi ya Rapid Wien siku iliyofuata.

### #3. GRANIT XHAKA (ARSENAL)

Granit Xhaka alikuwa na uwezo wa kuwa kiongozi mzuri wa Arsenal. Anajulikana kwa kucheza na kujitolea.

Kocha Unai Emery alimfanya Xhaka kuwa nahodha wa Arsenal kwa msimu wa 2019-20. Hata hivyo, mbio za mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi kama nahodha wa 'Washikabunduki' hao zilidumu kwa miezi miwili pekee. Xhaka alizomewa baada ya kufanya vibaya pale Emirates dhidi ya Crystal Palace.

Alipotolewa nje mashabiki walimzomea ambapo Xhaka alijibu kwa ishara ya kuwatusi na alivuliwa unahodha baada ya mchezo.

### #2. WILLIAM GALLAS (ARSENAL)

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, Arsenal ilikuwa na manahodha wawili wa Ufaransa waliofuatana. Patrick Vieira alikuwa kiongozi bora na Thierry Henry alikuwa mrithi wake. Hivyo Henry alipoondoka katika klabu hiyo, Arsenal waliamua kukabidhi kitambaa cha unahodha kwa Mfaransa mwingine William Gallas dhidi ya Gilberto Silva.

Lakini Gallas hakuweza kufuata nyayo za Vieira na Henry. Gallas alionekana kuchukizwa na mambo yaliyokuwa yakiendelea klabuni hapo na kuamua kugoma kwa kukaa uwanjani baada ya Arsenal kuruhusu bao la dakika za lala salama dhidi ya Birmingham City.

Ili kufanya mambo kuwa mabaya zaidi, Gallas aliwakosoa vijana wa klabu hiyo na kuzungumzia ugomvi kwenye chumba cha kubadilishia nguo cha Arsenal. Ilisababisha Mfaransa huyo kuondolewa katika nafasi yake kama nahodha...

## ISIKUPITE

NYOTA wa Bayern Munich, Thomas Muller ndiye mchezaji aliyetengeneza nafasi nyingi kubwa zaidi kwa kalenda ya mwaka 2021 barani Ulaya, akifanya hivyo mara 14, huku kwa ujumla pasi zake za mwisho ('assists') zikiwa ni 24, anafuatiwa na Filip Kostic wa Eintracht Frankfurt - nafasi kubwa 13 jumla ya 'assists' 17 huku akifuata Kylian Mbappe wa PSG - nafasi kubwa 12 na jumla ya assists 17.



### #1. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG (ARSENAL)

Arsenal walimvua kitambaa cha unahodha Granit Xhaka na kumpa Pierre-Emerick Aubameyang. Ilikuwa na maana kwa sababu Aubameyang alikuwa mchezaji bora wa 'Washikabunduki' wakati huo.

Kulikuwa na uvumi mwingi kuhusu uwezekano wake wa kuondoka, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon alikomesha uvumi huo kwa kusaini mkataba mnono. Lakini tangu kuongezewa mkataba wake, Aubamayeng alikuwa tofauti na alivyokuwa mwanzo.

Aubameyang aliwakasirisha mashabiki kwani uchezaji wake uwanjani haukuwa mzuri pia na kujitolea kwake kulitiliwa shaka mara kwa mara.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta aliamua imetosha mapema Desemba akaamua kumvua unahodha Aubamayeng.

Extra Time

# WACHEZAJI 10 WAKUTAZAMWA ZAIDI FAINALI ZA AFCON 2022



ÉDOUARD MENDY

**YOUNDE,** Cemroon

MICHUANO ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2022, ilianza jana Jumapili nchini Cameroon.

Michuano ya Afcon kwa hakika ndiyo yenye hadhi kubwa zaidi ya soka kwa bara la Afrika.

**Ukitazama kwa haraka Ligi Kuu England, Hispania, LaLiga na Bundesliga ambako wachezaji wengi wa Kiafrika wanacheza, baadhi ya klabu zitakuwa zinakosa huduma zao.**

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 wa kutazamwa zaidi kwenye michuano ya Mataifa ya Afrika nchini Cameroon 2022, hawa hapa...

### #1. MOHAMED SALAH - MISRI

Mohamed Salah bila shaka ndiye mwanasoka bora wa Afrika mwaka 2021 na mmoja wa wachezaji wa kuvutia zaidi katika misimu mitatu iliyopita. Akicheza kama mshambuliaji wa Liverpool, Salah alikuwa thabiti mbele ya lango.

Amekuwa bora na ameshirikiana na Mwafrika mwenzake, Sadio Mane ambaye ni mmoja wa wachezaji bora kwenye kikosi cha Liverpool kwa misimu mitatu iliyopita.

Bila shaka, Salah ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani, anayejulikana sana kwa umaliziaji wake, kupiga chenga na kasi.

Katika mechi zaidi ya 160 akiwa na Liverpool kwenye Ligi Kuu England, alifunga mabao 108 ya kuvutia kwa klabu hiyo.

Akiwakilisha Misri, Salah alimaliza Kombe la Mataifa ya Afrika lililoandaliwa na Gabon mwaka 2017 kama mshindi wa pili. Alifunga mabao mawili kwenye michuano hiyo.

Baadhi ya mataji aliyotwaa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super Cup, Klabu Bingwa Dunia, Ligi Kuu England na ubingwa wa Ligi Kuu ya Uswisi.

### #2. NABY KEÏTA - GUINEA

Kushikilia kwa uthabiti nafasi ya kiungo wa kati kwenye Ligi Kuu England si rahisi zaidi hasa katika klabu kama Liverpool ambapo ushindani uko kwenye kilele chake. Lakini Keïta ameshikilia nafasi yake pale kwenye dimba la Anfield.

Keïta ambaye alianza maisha yake ya soka katika klabu ya Ligi Daraja la Pili nchini Ufaransa katika Klabu ya FC Istres, alihamia Leipzig ambako ushujaa wake ulivutia hamu ya Liverpool.

Ingawa ushindani wa Liverpool kwa sasa uko kwenye kilele chake kwa Keita, hajashindwa kufanya lolote anapokuwa uwanjani.

Uwezo wake mkuu ni zaidi ya kusambaza pasi sahihi na kushika nusu yake ambapo kuna mashambulizi kwenye nafasi yake.

Kufikia sasa baadhi ya tuzo ambazo Keita ameshinda ni pamoja na Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya,

Klabu Bingwa Dunia na Ligi Kuu ya Austria.

### #3. YVES BISSOUMA - MALI

AFCON inaahidi furaha zaidi huku Yves Bissouma akisimama kama ngome ya timu ya Taifa ya Mali.

Bissouma ni kiungo mbunifu ambaye amekuwa kwenye vitabu vya Brighton & Hove Albion ya Ligi Kuu England tangu mwaka 2018 na kwa sasa ni mmoja wa viungo wanaosakwa sana sokoni.

Ufungaji wa bao si lengo la Bissouma, bali uwezo wake ni zaidi katika uchezeshaji timu ambao unajumuisha usambazaji wa pasi nzuri.

Jukumu lake kuu katika klabu ya Brighton Hove Albion ni eneo la kiungo au sawa na kiungo mkabaji, ambaye kazi yake ni kulinda beki.

Jambo moja zuri kuhusu Mali ambayo imemfanya kuwa mmoja wa wachezaji bora wa klabu hiyo ni uthabiti wake.

Bissouma ni mmoja wa wachezaji bora wa kiungo wa kutazamwa katika Kombe la Mataifa ya Afrika nchini Cameroon.

### #4. KALIDOU KOULIBALY - SENEGAL

Kalidou Koulibaly, kwa sasa ndiye beki bora katika bara la Afrika. Tangu alipotua Napoli mwaka 2014, tayari amejipatia jina katika Ligi Kuu Italia, Serie A.

Koulibaly ameichezea Napoli zaidi ya mechi 221 kwenye ligi na amefunga mabao 12.

Tangu mwaka 2014, ameunda ukuta mzuri nyuma wa Napoli ambao kwa sasa ndio msingi wa mafanikio ya timu hiyo tangu kuanza kwa msimu 2021/2022.

### #5. FRANCK KESSIE - IVORY COAST

Franck Kessie amejitengenezea jina maarufu kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na AC Milan.

Akiwa kama sehemu kamili ya kikosi cha vijana cha AC Milan cha kocha Stefano Pioli, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast amekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya Milan kwenye misimu miwili iliyopita.

Akihamia AC Milan mwaka wa 2017, Kessie amekuwa bora ikiwa ni pamoja na kuisaidia klabu hiyo kupata nafasi ya pili kwenye Serie A msimu wa 2020-21 na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2021-22.

Akianza Ligi ya Mabingwa akiwa na Milan baada ya miaka nane ya kutokuwapo, Kessie alikuwa bora.

Alicheza mechi tano kati ya sita za hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Katika Série A, yeye ni mmoja wa wachezaji waliofanya vizuri zaidi kwenye klabu na ana mabao matatu.

Kessie pamoja na Sébastien Haller, Wilfried Zaha, na Nicolas Pepe wanatarajiwa kuongoza kikosi cha Ivory Coast pengine hadi fainali.

### #6. SADIO MANÉ - SENEGAL

Anaunda safu ya utatu ya mbele ya Liverpool tangu mwaka 2016, Mane alikuwa mwanajeshi na jicho la tai katika Ligi Kuu England akiwa na Liverpool.

Mané aliisaidia Liverpool kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya sita mwaka 2019, baada ya kushindwa na Real Madrid katika fainali iliyopita mwaka 2018.

Mane anajulikana kwa kasi yake ya juu na mbio na amekuwa miongoni mwa wachezaji bora wa Liverpool katika misimu michache iliyopita.

Mané anaweza kuelezewa kama mfungaji mabao hodari, akiwa na uwezo wa kipekee kama vile kumalizia, kasi na kumiliki mpira.

Baadhi ya tuzo za Mane ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ligi Kuu England, Klabu Bingwa Dunia, UEFA Super na Ligi Kuu ya Austria.

#7. Riyad Mahrez - Algeria

Riyad Mahrez ni mmoja wa wafungaji wa mabao kwa kasi na mahiri katika bara la Afrika.

Raia huyo wa Algeria anayechezea Manchester City alifunga mabao matatu ikiwa ni pamoja na nyota watano kuisaidia nchi yake kutwaa ubingwa wa Afcon kwa mara ya pili baada ya miaka 31.

Mahrez chini ya kocha Pep Guardiola katika klabu ya Man City amekuwa mchezaji hodari zaidi, ambaye ana uwezo wa kucheza popote pale mbele. Uwezo wake unamfanya kuwa mmoja wa wachezaji bora katika Ligi Kuu England.

Kwa sasa, anachukuliwa kuwa mmoja wa mawinga bora zaidi katika kandanda ya dunia ambayo inaweza kutokana na mafanikio aliyoyapata alipokuwa Man City chini ya Guardiola.

Akiwa na timu ya taifa, Mahrez pamoja na Ismaël Bennacer walisaidia Algeria kutwaa Kombe la Mataifa ya Afrika mwaka 2019 kwa kuwashinda Senegal.

Mahrez ni miongoni mwa nyota wakubwa wanaotarajiwa kutazamwa kwenye Afcon.

### #9. WILFRED NDIDI - NIGERIA

Wilfred Ndidi ndiye mchezaji asiyebadilika zaidi wa Nigeria katika misimu mitatu iliyopita. Akiwa na Leicester City kwenye Ligi Kuu England, Ndidi amekuwa ngome ya kati kwa Mbweha hao ambaye pia ana uwezo wa kucheza nyuma.

Kiungo huyo anafahamika kwa umahiri wake wa safu ya ulinzi na mashambulizi ya muda mrefu ambayo yamemfanya kuwa miongoni mwa wachezaji wanaozungumzwa zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Tangu mwaka 2017, Ndidi alikuwa amejiweka kama moja ya chaguzi zinazopendekezwa zaidi kwa Leicester katika mashindano yote.

Msimu wa 2020/2021, Mnigeria huyo aliisaidia Leicester kushinda Kombe la FA dhidi ya Chelsea na Ngao ya Jamii dhidi ya Manchester City. Ndidi ameendelea kudumisha msimamo wake wa kawaida katika klabu hiyo. Ni mmoja wa wachezaji bora wa kuwatazama kwenye Afcon.

### #10. ÉDOUARD MENDY - SENEGAL

Édouard Mendy ndiye mlinda mlango bora zaidi katika bara la Afrika kwa sasa.

Akihama kutoka klabu ya Ligi Kuu Ufaransa, Rennes hadi Chelsea, Msenegal huyo haraka alijidhihirisha kuwa chaguo bora la kulinda goli kwa klabu hiyo yenye maskani yake jijini London.

Chelsea wakati huo walikuwa na alama ya maswali juu ya Kepa Arrizabalaga. Kwa Mendy, ilikuwa ndoto iliyotimia wakati alipocheza mechi 16 bila kuruhusu bao katika msimu wake wa kwanza wa Ligi Kuu akiwa na klabu hiyo.

Mwaka 2021, kwa kutambua uchezaji wake, Mendy alitunukiwa tuzo ya golikipa bora wa mwaka wa Uefa.

Mendy ameshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super Cup, na Ligue 2.

## Nukuu


"Leo ningesema kwamba ni bora zaidi kimwili [kuliko Cristiano Ronaldo], kwa sababu nilicheza hadi nilipotimiza umri wa miaka 43. Akifanya hivyo, nitasema ni yeye. Sina tabia mbaya. Sinywi pombe, sivuta sigara, nakula vizuri sana, nalala vizuri. Nina familia yangu, ambayo ni ulinzi wangu mkuu. Nadhani hayo ni mambo muhimu kufikia umri niliofikia na bado niendelee kucheza kwa kiwango cha juu," **Nyota wa zamani wa Brazil, Ze Roberto mwenye umri wa miaka 47, akilinganisha ubora wake kimwili na Cristiano Ronaldo wa Man United.**



"Maadam niko hapa katika 'Borussia Chelsea' yangu, sitafanya kitu kingine zaidi ya kufanya timu zingine zicheze chini ya kiwango. Tutajaribu hata kuifanya Manchester City kucheza chini ya kiwango. Hatutaacha. Na Jurgen (Klopp), nina uhakika atafanya vivyo hivyo kupata matokeo bora kutoka kwa Liverpool - na sisi hapa tutapata bora kutoka kwa Chelsea. Hatutaacha kufukuza. Hatutaacha kuamini au kuacha kufanya hivi," **Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel, akizungumzia mbio za ubingwa England wakati huu City ikiwa kileleni.**



"Nina heshima isiyo na mwisho kwa wote wawili na ninatazamia kuboresha mchezo wangu chini ya wafanyakazi wa Manchester United. Sijachukia, sijakosa furaha, je, nimekatishwa tamaa kwa kiwango changu cha sasa? Bila shaka. Mimi ni mkosoaji wangu mkuu. Umekuwa mwanzo mgumu, lakini nimedhamiria kuthibitisha thamani yangu. Kujitolea kwangu na hamu yangu ya kuwa hapa hakupaswi kuulizwa. Naipenda klabu hii," **mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford**





Winga mpya wa Yanga, Denis Nkane.

Kiungo anayefanya majaribio Simba, Etop Udoh David.

# NYOTA WAPYA WALIVYOGEUKA KIVUTIO MAPINDUZI CUP 2022

**Na Mwandishi Wetu**

MICHUANO ya Kombe la Mapinduzi itaendelea kutimua vumbi leo kwenye Uwanja wa Amaan Zanzibar hatua ya nusu fainali, Yanga ikicheza dhidi ya Azam na Simba ikikipiga na Namungo FC.

Awali, ilizishirikisha jumla ya timu 10 kutoka Bara na Visiwani, zilizoganyanyika makundi matatu, A likiwa na timu nne ambazo ni Azam FC na Namungo kutoka Bara na Yosso Boys na Meli Nne City kutoka Zanzibar.

Kundi B lilikuwa na timu za Yanga kutoka Bara, Taifa Jang'ombe na KMKM kutoka Zanzibar, huku Simba ya Bara na Selem View na Mlandege za Zanzibar zikiwa Kundi C.

Mara nyingi huwa ni michuano ambayo klabu hujaribisha wachezaji wa kuwasajili kipindi cha dirisha dogo kwa sababu hufanyika wakati huo, na wengine wanakuwa tayari wameshasajiliwa.

Mwaka huu, klabu mbalimbali zikiwamo Simba na Yanga zimekwenda na wachezaji wapya kwenye timu zao, wengine wakiwa tayari wamesajiliwa na baadhi wakifanya majaribio.

Baadhi yao wameshaanza kuuwasha moto na kuwa kivutio kikubwa huko, huku wengine bado wakiwa wanatafuta namba.

Hebu tuwaangalie baadhi ya wachezaji wapya ambao wapo Zanzibar kwenye michuano ya Kombe hilo la Mapinduzi...

**DENIS NKANE - YANGA**

Tayari amesajiliwa na klabu ya Yanga, na kwenye mechi yake ya kwanza tu ametupia. Alifunga bao la pili Jumatano iliyopita, Yanga ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Taifa Jang'ombe ya Zanzibar.

Ameonekana kuanza na moto, kwani licha ya kufunga bao, lakini alikuwa mwiba mkali kwa mabeki wa timu pinzani. Hata hivyo, alidhibitiwa kwenye mechi ya pili dhidi ya KMKM na hakufurukuta.

Nkane anayecheza winga ya kulia anategemewa kufanya makubwa kwenye klabu hiyo, na amejiunga na ya Yanga kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, akitokea Biashara United.

**CHEIK MOUKORO - SIMBA**

Ni winga raia wa Ivory Coast aliyekuja nchini kwenye klabu ya Simba kwa ajili ya kufanya majaribio.

Dakika chache tu alizoingia kwenye mechi ya Jumatano jioni katika Uwanja wa Amaan Zanzibar, akiwa na kikosi cha Simba kilichotoka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Selem View ya Zanzibar, alionyesha ana kitu mguuni.

Kwa muda mfupi aliocheza, aligeuka kuwa kivutio kikubwa cha mashabiki waliofurika kwenye uwanja huo, kwanza kabisa kutokana na kasi yake, wepesi, uwezo wa kupiga chenga za maudhi akitumia mguu wa kushoto. Lakini kikubwa zaidi ni kuweza au uthubutu wake wa kupiga mashuti, kwani licha ya kuingia katikati ya kipindi cha pili, lakini Moukoro alipiga mashuti yapatao manne, tena ya hatari na kuwazidi hata baadhi ya wachezaji ambao walicheza dakika zote 90.

**CRISPIN NGUSHI - YANGA**

Straika huyu naye pia ilikuwa ni mechi yake ya kwanza kuichezea Yanga, akitokea Mbeya Kwanza. Kwenye Ligi Kuu ana mabao matatu aliyoyafunga akiwa na timu yake ya zamani. Amesajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo. Jumatano iliyopita kwenye mechi dhidi ya Taifa Jang'ombe ilikuwa ya kwanza kwake kuitumikia timu mpya, lakini hakufanya vizuri sana kama mwenzake Nkane.

Alionekana kutaka kufanya vitu vingi vigumu kwa wakati mmoja kutaka kuwadhihirishia wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa hawakufanya kosa kumsajili. Hakucheza kwenye mechi iliyofuata dhidi ya Mlandege.

**SHARAF ELDIN SHIBOUB - SIMBA**

Si mchezaji mgeni sana kwenye klabu ya Simba. Misimu kadhaa nyuma aliichezea timu hiyo kabla ya kutimka. Amerejea tena, ikielezwa kuwa anakuja kufanya majaribio ili kama akionekana yuko vizuri asajiliwe.

Aliingia kipindi cha pili na mwenzake Moukoro kwenye mechi ya Jumatano jioni dhidi ya Selem View. Tofauti na mwenzake ambaye aliupiga mwingi, Shiboub hakuonekana kucheza vizuri sana wala vibaya. Labda kutokana na aina yake ya uchezaji wa taratibu. Anayesubiriwa ni Kocha wa Simba, Pablo Franco kutoa idhini kama asajiliwe au la, huku kukiwa pia na taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba kuwa mchezaji huyo alikuja kama mwalikwa na si kwa ajili ya kusajiliwa.

**IBRAHIM AJIBU - AZAM**

Kama ilivyosemwa huko juu kuwa Ajibu alianza kujulikana kwenye ulimwengu wa soka kupitia michuano hii, akiwa na Simba mwaka 2017, ilikuwa imemrejesha kutoka kucheza kwa mkopo Mwadui FC, akiwa mchezaji wa kikosi cha pili. Kwenye michuano hiyo aling'ara na kuiwezesha Simba kutwaa kombe hilo, na baada ya hapo moja kwa moja akawa mchezaji wa kikosi cha kwanza.

Jumanne iliyopita alikuwa mmoja wa wachezaji wapya wa Azam FC, akiiongoza vema kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Meli Nne City ya Zanzibar, akicheza kwa mara ya kwanza kwenye klabu hiyo akitokea kwenye timu yake ya zamani ya Simba.

**ETOP UDOH DAVID - SIMBA**

Hana mbwembwe, bali ni mchezaji anayejua kupora mipira, kupiga pasi ndefu, fupi na hata kupiga mashuti.

Huyu ni raia wa Nigeria ambaye pia amekwenda Zanzibar na Simba kufanya majaribio. Ni mchezaji wa nguvu na misuli na anacheza kama kiungo mkabaji. Wataalamu wa masuala ya soka wanadai ni mchezaji mzuri kutokana na namba anavyoicheza, lakini mashabiki ambao wengi hupenda zaidi wachezaji wenye kupiga chenga, matobo na kanzu, bali wana wasiwasi naye. Alicheza mechi ya Simba dhidi ya Mlandege, akiingia kipindi cha pili.

**JE, WAJUA?**




Neymar ambaye kwa sasa anaichezea Paris Saint-Germain ya Ufaransa, ndiye mchezaji kutoka Brazil mwenye mabao mengi zaidi (41) kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kuliko mchezaji yeyote kutoka nchini humo, akifuatiwa na Ricardo Kaka mabao 30 na Rivaldo aliyecheka na nyavu mara 27.







Mmoja wa wanafamilia akiwaonyesha sehemu ya vyumba vilivyoteketea kwa moto usiku na kusababisha hasara kwenye nyumba inayomilikiwa na Bashiru Shilla mkazi wa mtaa wa Bonanza, jijini Dodoma, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# RC Mtaka atoa angalizo miradi UVIKO-19

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, amewataka makandarasi wanaotekeleza miradi ya maji inayofadhiliwa na fedha za UVIKO-19, kukamilisha kwa wakati na kwa ufanisi.

Mtaka, aliyasema hayo jijini hapa juzi wakati wa hafla fupi ya kusaini mikataba ya ujenzi wa miradi ya maji kati ya makandarasi na mamlaka ya maji vijijini (RUWASA), Mkoa wa Dodoma.

Alisema kuwa mkandarasi atakaye tekeleza miradi hiyo chini ya kiwango na nje ya mkataba, mkoa hautampatia kazi nyingine. "Niseme tu kwamba kwa mkandarasi atakayeshindwa kutekeleza miradi yake kwa muda na kwa ufanisi hatutampatia kazi tena (tuta-blacklist) kwa kuwa lengo ni kwamba kwenda na kasi ili kazi zikamilike mapema," alisema Mtaka.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga alisisitiza miradi hiyo ifanyike kwa ufanisi na kwa kiwango cha thamani ya fedha iliyotolewa ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuwaletea wananchi wake maendeleo.

Awali, akisoma taarifa fupi ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa Mkuu wa mkoa, Meneja wa RUWASA Mkoa, Dk. Godfrey Mbabaye, alisema mikataba inayosainiwa imegawanyika katika makundi mawili.

Alisema Mkoa wa Dodoma ulitengewa Sh. bilioni 3.9 kutekeleza miradi nane, katika wilaya za Kongwa, Chamwino, Kondoa, Chemba na Mpwapwa.

"Mikataba inayotarajiwa kusainiwa leo ni miwili ya wilaya za Chamwino, Chemba na Kondoa yenye jumla ya miradi mitano na thamani yake ni Sh. bilioni 1.9," alisema Mbabaye.

Alisema mkataba mmoja wenye miradi mitatu ya wilaya ya Kongwa na Mpwapwa wenye thamani ya Sh. bilioni 1.6 umepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa serikali kwa ajili ya kufanyia upembuzi na unategemewa kusainiwa kabla ya Januari 16, 2022.

"Miradi inayotumia fedha za ndani inayotegemewa kusainiwa leo ni miwili ambayo itatekelezwa katika wilaya za Chamwino na Kondoa na ina jumla ya Sh. bilioni 1.7," alisema Mbabaye.

# SUMA JKT yabanwa kuharakisha miradi ujenzi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Ujenzi la SUMA JKT limepewa Sh. bilion 7.5 kwa ajili ya ujenzi wa shule ya mfano ya Sekondari Iyumbu iliopo jijini hapa inayotarajia kukamilika Agosti, mwaka huu.

Kwa mujibu wa makubaliano, shule hiyo ilitakiwa kukamilika Februari mwaka huu, lakini imeshindikana kutokana na SUMA JKT kushindwa kukamilisha kwa sababu ya changamoto mbalimbali za ujenzi zilizojitokeza. Akizungumza juzi na waandishi wa habari katika ziara ya kutembelea majengo hayo pamoja na Chuo cha Ufundi Stadi, aliyekuwa Waziri wa Elimu Prof. Joyce Ndalichako, alisema ni ongezeko la mwisho la muda wa ujenzi wa shule hiyo kwa sababu hawana sababu ya kuchelewa kukamilisha ilhali fedha zipo.

Hata hivyo, alisema hatawapa miradi mingine mpaka watakapokamilisha huo kwa sababu wamekuwa wakichelewesha miradi ya elimu tofauti na miradi mingine wanayokabidhiwa kujenga. Ndalichako alisema kuanzia sasa anasimisha SUMA JKT kupewa mradi wowote wa ujenzi wa Wizara ya Elimu kwa sababu wanaikwamisha.

Akifafanua, alisema zaidi ya kuwa shule sekondari ya Mfano Iyumbu iliyokuwa ikamilike Februari, mwaka huu mpaka sasa ujenzi uko asilimia 55 na sehemu iliyobaki ni kubwa kulingana na muda uliobaki.

"Kwa Kweli SUMA JKT mnanikatisha tamaa sana kwa sababu nyie ni serikali kwanini mrudishe nyuma maendeleo katika ujenzi?" Alihoji Prof. Ndalichako.

Aliitaja miradi ambayo wameikwamisha ni pamoja na ujenzi maabara mtambuka katika Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA), mabweni katika Chuo cha Mzumbe na Chuo cha Ualimu Kabanga, jambo ambalo linamtoa imani ya kuwaamini SUMA JKT kama watamaliza ujenzi wa shule hiyo kwa wakati.

Alisema mkandarasi huyo amejenga tabia ya kuomba waongezewe muda jambo ambalo amekuwa akilifanya kwenye miradi hiyo yote iliyotajwa.

"Sisi wote ni serikali hivyo tusiangushane. Tunapaswa kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwa ametoa fedha nyingi katika elimu, hivyo nanyi mnapaswa kufanya kazi kwa bidii," alisisitiza Ndalichako.

Akitoa taarifa ya Mradi huo Meja Geoffrey Ngole alisema umekamilika kwa asilimia 55 na mabweni ni asilimia 60, bwalo asilimia 85, nyumba za walimu pia ni asilimia 85.

Alisema gharama za ujenzi huo ni Sh. bilioni 17.1 na mpaka sasa fedha za matumizi walizopata ni Sh. bilioni 7.5.

Hata hivyo, alisema moja ya changamoto zilizochelewesha ujenzi huo ni kukosa vifaa ambavyo havikufika kwa wakati na kuchangia kuchelewesha.

Meja Ngole alisema wako tayari kutekeleza kile walichoagizwa na Waziri wa Elimu ili shule hiyo ikamilike.

Akizungumzia kuhusu mradi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Dodoma, Waziri Ndalichako alisema ameridhishwa na ujenzi huku akiwasisitiza kuendelea na kasi hiyo ili wamalize kwa wakati uliopangwa.

Kuhusu changamoto za upatikanaji maji na umeme, Ndalichako ameahidi kuzungumza na Waziri wa Maji na wa Nishati ili kuhakikisha wanapata huduma hizo kwa haraka na mradi uweze kuendelea. Akiongea kwa niaba ya Mkandarasi wa chuo hicho, CRJE Company Limited, Mhandisi John Kyara alisema mpaka sasa ujenzi umekamilika kwa asilimia 30 na kwamba wanaamini mradi utakamilika kwa wakati uliopangwa.

# Waomba kutungwa sheria bima afya kwa wote

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

VIONGOZI wa Taasisi za kidini nchini wameishauri serikali kuharakisha mchakato wa kutungwa kwa sheria ya bima ya afya kwa wote ili kuwapunguzia wananchi mzigo wa matibabu wakati wanapokuwa wagonjwa.

Mwenyekiti wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na Mwenyekiti mwenza wa Kamati ya Viongozi wa dini mbalimbali nchini, Shekhe Khamisi Saidi Mataka, alitoa ushauri huo mwishoni wa wiki wakati alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Mataka alisema viongozi hao wanashauri serikali kuharakisha mchakato wa kutunga sheria ya bima ya afya ili kuwapunguzia mzigo wa gharama za matibabu wananchi.

"Sisi viongozi wa Taasisi za dini nchini tunasema kuwa sheria ya bima ya afya kwa watu wote sasa ipitishwe ili kuwapunguzia wananchi wetu gharama za matibabu," alisema.

Alisema kuanzishwa kwa sheria hiyo michango ya fedha itaongezeka na kusaidia watu wengi kunufaika na huduma za matibabu.

Vile vile, alisema Taasisi hiyo ya kidini inaundwa na washirika wa maendeleo ya kidini ambayo ni Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) TEC, BAKWATA na Tume ya Kikristo ya huduma za kijamii (CSSC).

Ilifanya utafiti kuhusu huduma za afya nchini, ulizinduliwa mwaka 2018 na unajulikana kwa jina la tufanye afya kwa wote (Make it possible).

Utafiti huo ulikuwa na malengo ya kujua hali ya utoaji na ufikiwaji wa huduma za afya nchini, ushiriki wa taasisi na viongozi wa dini nchini katika kuchangia uboreshaji wa huduma za afya.

Alisema baada ya matokeo hayo kamati ya viongozi wa dini mbalimbali wamepewa jukumu la kushauri na kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujiunga na bima hiyo.

Mratibu wa Kamati hiyo, Edmund Matotay, alisema kwa wastani uchangiaji katika sekta ya afya unaonyesha kuwa serikali inachangia asilimia 35, wadau wa maendeleo 37 na watoa huduma binafsi 28.

Kamati hiyo na viongozi wa dini wanajukumu la kuwaelimisha waumini wa dini zao kuunga mkono juhudi za serikali katika mchakato wa kupitisha sheria hiyo ya bima ya afya kwa watu wote.

Naibu Katibu Mkuu Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Chesco Msaga, alisema wanaridhishwa na serikali kuona mwendelezo wa dhamira nzuri kuhakikisha bima ya afya inapatikana kwa kaya maskini nchini.

Alisema serikali imewekatia bima ya afya ya CHF wananchi hao maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Aidha alisema kwa muda wa miaka minne tangu kuzinduliwa kwa utafiti wao wanaendelea na kampeni ya kuwahamaisha wananchi kujiunga na bima ili kuwasaidia wakati wa ugonjwa.





## Miche milioni 1.6 kupandwa kukabiliana mabadiliko tabianchi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WILAYA ya Rungwe, mkoani Mbeya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imejipanga kutoa zaidi ya miche milioni 1.6 ya mbao, matunda na kivuli ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kuhifadhi mazingira wilayani humo.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Castor Makeula, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu maandalizi ya utaoji wa miche kwa wananchi.

Makeula alisema miche hiyo itagawiwa bure kwa wananchi kwenye sekta binafsi na umma kuwezesha wananchi kujikwamua kiuchumi kupitia biashara ya mbao na matunda.

"Tumeamua kuzalisha miche 1.6 ya aina mbalimbali kama vile matunda, mbao na kivuli ikiwa ni hatua ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kilimo na kukuza biashara ili kukuza uchumi wa wakazi wa Rungwe sambamba na utunzaji wa mazingira," alisema Makeula.

Baadhi ya wananchi walisema ni utaratibu mzuri ulioanzishwa na wilaya kuwagawia miche ili kuendeleza jitihada za kuhifadhi mazingira na wataendelea kuitunza kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

Miongoni mwa wananchi hao, Mary Mwangupili wa kijiji cha Ilolo, alisema ni mara kadhaa amekuwa akipewa miche ya matunda na mbao na viongozi wa wilaya hiyo na kwamba ameanza kunufaika kwa kuuza parachichi na kujiingiza kipato.

Aliishukuru serikali na kuishauri kuongeza jitihada kutunza chanzo cha maji cha Mto Kilasi ili kiendelee kutoa maji katika kipindi chote cha mwaka na kupanda miti.

# Mamia wamzika mwandishi Sikagonamo

**Na Grace Mwakalinga,** BUSOKELO

MAMIA ya wakazi wa ndani na nje ya Mkoa wa Mbeya, wamejitokeza kwenye mazishi ya aliyekuwa Mwandishi wa Habari wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya na Mkurugenzi wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Elimisha, Festo Sikagonamo.

Mazishi ya marehemu Sikagonamo yalifanyika juzi kijiji kwao Kilugu kata ya Itete Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali pamoja na wadau waliofanya kazi kwa karibu na marehemu.

Sikagonamo alifikwa na umauti usiku wa kuamkia Januari 7, mwaka huu, akiwa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH) baada ya kulazwa hospitalini hapo kwa wiki moja kwa matatizo ya kifua kwa mujibu wa familia.

Miongoni mwa viongozi walioshiriki mazishi hayo ni Mbunge wa Jimbo la Songwe, Philip Mulugo ambaye alisema marehemu alichangia kwa kiasi kikubwa kupata ubunge kupitia habari mbalimbali alizomwandikia.

Alisema mchango wa marehemu Sikagonamo katika tasnia ya habari ulikuwa mkubwa na utakumbukwa kwa namna alivyokuwa akitekeleza majukumu yake kwa weledi na ubunifu.

"Msiba huu umeniumiza sana Sikagonamo alikuwa mtu wangu wa karibu alichangia kwa kiasi kikubwa kupata ubunge huu, nasikitika imekuwa ghafla maana sijasikia kuumwa kwake hakika nitamkumbuka ndugu yangu, rambirambi yangu ya Sh. 500,000 isaidie watoto wa marehemu shuleni," alisema Mulugo.

Mkuu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kutoka TBC, Gift Ambwene, alisema shirika hilo limempoteza mfanyakazi mahiri, mbunifu, mtiifu na aliyefanya kazi kwa kujitoa na pengo lake kamwe haliwezi kuzibika.

Alisema TBC imetoa Shilingi milioni tatu kwa ajili ya kufanikisha mazishi ya marehemu Sikagonamo na wameupokea kwa uzito mkubwa. Akizungumza kwa niaba ya Chama cha Wanahabari Mkoa wa Mbeya, Ulimboka Mwakilili, alisema miongoni mwa alama alizoacha Sikagonamo ni kuanzia mkakati wa kutoa elimu ya upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia.

Alisema programu hiyo ilipokelewa kwa mikono miwili na wananchi na iliwasaidia kupanga bajeti na kujikwamua kiuchumi.

Marehemu Festo Sikagonamo amefariki akiwa na umri wa miaka 43, ameacha mke na watoto watatu ambao ni Grace, Ushindi na Gabriel.




Mkuu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Gift Ambwene, akiweka shada la maua kwenye kaburi la marehemu Festo Sikagonamo ambaye alikuwa mtumishi wa shirika hilo, mazishi yaliyofanyika katika kijiji cha Kilugu, Halmashauri ya Busokelo mkoani Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbunge kukarabati barabara zilizoharibiwa na mvua

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, amewaahidi wananchi wa Kata ya Nsalaga kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Mbeya kukarabati miundombinu ya barabara kutokana na mvua iliyonyesha na kusababisha mafuriko eneo hilo.

Dk. Tulia aliyasema hayo jana alipowatembelea wakazi wa Mtaa wa Itezi, Kata ya Nsalaga kwa lengo la kutoa pole baada ya kukumbwa na mafuriko.

"Leo tumekuja kuangalia athari zilizojitokeza ili tuweze kuona ni namna gani tutaweza kuzitatua, naamini wakala wa barabara mijini na vijijini TARURA watarekebisha miundombinu hii ili irejee kwenye hali yake ya kawaida sambamba na Idara ya Maji pia tunaomba msaada wao alisema Dk. Tulia.

Aliongeza kuwa leo timu ya wataalamu ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya watafika kwa ajili ya kufanya ukaguzi na kuweka mikakati ya namna miundombinu hiyo itajengwa.

Pia, aliahidi kuwapatia kilo 100 za mchele familia zilizoathirika na mafuriko pamoja na maharagwe na kwamba bidhaa hizo atazikabidhi kwa mwenyekiti wa mtaa ambaye anawafahamu waathirika.

Aliwashauri wakazi wa Itezi kuacha kulima pembezoni mwa mito kwa madai kuwa shughuli hizo zinasababisha mto kuendelea kutanuka na maji kuacha njia na kuleta mafuriko kwenye makazi ya watu.

Baadhi ya wananchi waliokumbwa na mafuriko akiwamo Jasmine Abdalla, alisema kila mwaka wanakumbwa na mafuriko kutokana na miundombinu ya maeneo hayo kutokuwa imara na kuomba serikali kujenga miundombinu imara ikiwamo barabara na madaraja ili kuondokana na mafuriko kila msimu wa mvua za masika.

Alimshukuru mbunge kwa kuwatembelea na kujionea hali halisi na kuwaahidi kushughulikia miundombinu iliyoharibika na kuwapatia msaada wa chakula waathirika wa mafuriko.



# Viwanda vidogo vya kati kutoa ubora bidhaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KUIMARIKA kwa viwanda vidogo na vya kati kutaviwezesha viwanda hivyo kutoa huduma zenye ubora na kuzalisha bidhaa zenye kukidhi ushindani katika soko la ndani, kikanda na kimataifa.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said, baada ya kuweka jiwe la msingi jengo la makao makuu ya Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo na kati (SMIDA) Maruhubi, Zanzibar.

Alisema malengo makuu ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuleta usawa na kuweka mazingira bora ya utoaji huduma kwa wananchi wote ili kujikwamua kiuchumi, kijamii na kisiasa. Alisema kukamilika kwa jengo hilo kutasaidia kuimarisha huduma za wajasiriamali na wazalishaji wa bidhaa nchini.

Aidha, alisema itasaidia kupatikana kwa ajira endelevu na kuongezeka kwa thamani ya biashara.

"Naipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa utekelezaji ya maagizo ya Rais, leo hii tunayo SMIDA tuitakayo ambayo inaendelea kuweka mazingira mazuri ya uendeshaji wa viwanda hasa venye kutumia malighafi za ndani, kutokana na mazao ya kilimo, mifugo na mazao ya baharini, ikiwamo dagaa na mwani ili kuimarisha uwekezaji wa ndani, katika kuanzishwa na kuendeleza viwanda nchini," alisema Simai.

Alisema matarajio yake, SMIDA itaendelea kusaidia katika upatikanaji wa maeneo ya pamoja ya uzalishaji wa viwanda, huduma za kifedha na mitaji pamoja na utafutaji wa masoko kwa wajasiriamali na kuwajengea uwezo wazalishaji wa sekta ya viwanda kwa kuwapatia mafunzo, kujenga ubunifu na kuleta teknolojia za kisasa katika sekta ya uzalishaji na viwanda.

"Tuna kila sababu na haki ya kujivunia ujenzi wa Ofisi za SMIDA kwa kuzingatia kuwa Serikali ya Zanzibar ndiyo inagharamia Sh. 3,124,052,301 zinazotokana na fedha za maendeleo (Development Fund). Haya ndiyo matunda ya Mapinduzi, leo Zanzibar imeondokana na utegemezi." Aliwataka wafanyakazi wa SMIDA kuwa wabunifu kuhakikisha taasisi inaibua miradi mipya yenye tija na kuongeza uwapo wa viwanda vidogo na vya kati.\

Naye Mkurugenzi wa SMIDA, Soud Said Ali, alisema changamoto kubwa inayoikabili wakala ni ufinyu wa nafasi katika ofisi zake za sasa na kusababisha kukosekana kwa ufanisi katika utendaji wa kazi zake.

Pia alisema wakala haina eneo moja la uzalishaji (Common facility/Processing Center) ambalo lingeweza kuwaweka pamoja wazalishaji wengi wa viwanda na kuzalisha bidhaa zenye ubora zinazokidhi mahitaji ya masoko ya ndani na nje.

"Tukiwa tunaweka jiwe la msingi la jengo letu hili kwa lengo la kuboresha huduma zetu wakala bado inakabiliwa na upungufu wafanyakazi hususan wahandisi wa viwanda kama vile wa usindikaji wa chakula, wahandisi wa viwanda na wa umeme na mitambo," alisema mkurugenzi huyo.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara Maendeleo na Viwanda, Dk. Islam Seif, alisema Zanzibar inategemea maendeleo ya viwanda vidogo na vya kati ndiyo sahihi na inazingatia suala la mazingira.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Said Muhammed (kushoto), akisalimiana na Mkurugenzi wa Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Kati (SMIDA), Soud Said Ali, alipofika kwa ajili ya kuweka jiwe la msingi jengo la makao makuu ya SMIDA Maruhubi. **PICHA: SALMA SULAIMAN**

## Othman aeleza umuhimu wa rasilimali nchini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni muhimu kwa wafanyabiashara kutumia fursa za rasilimali zilizoko kuwekeza katika uzalishaji wa viwanda.

Aliyasema hayo viwanja vya Masira mjini hapa alipofungua tamasha la nane la maonyesho ya biashara.

Alisema viwanda vinavyoanzishwa ni vyema vilenge katika kuzalisha bidhaa bora zinazozingatia viwango vya kimataifa kwa kusarifu na kuongeza thamani ya bidhaa hizo kwa uzalishaji wa mafuta, arki na dawa zinazoweza kutumika kwa masoko ya ndani na nje ya Tanzania.

Vile vile, alisema kuna haja kwa wizara inayoshughulikia masuala ya biashara na maendeleo ya viwanda Zanzibar kuwa na mkakati madhubuti wa kuhamasisha jamii kupenda kununua na kutumia bidhaa za ndani.

Kwa upande mwingine, Othman alishauri kukutanishwa wadau wa biashara na maendeleo ya kiuchumi ili kubadilishana mawazo kwa nia ya kukuza uchumi na maendeleo ya Zanzibar.

Alisema hatua hiyo pia ni kutoa nafasi kwa wadau wa biashara, viwanda, kilimo na utalii kwa pamoja kubaini fursa mpya za kiuchumi zilizopo sambamba na kutambua huduma zinazotolewa zilivyoboreshwa ikiwa ni jitihada za kuharakisha maendeleo nchini.

Alishauri vyema tamasha hilo la biashara kutoka ngazi ya kitaifa na kikanda hadi kuwa ya kimataifa ili watu wengi zaidi wajumuike kujionea na kutumia fursa za biashara na kiuchumi na kuharakisha kuleta maendeleo ya taifa.

Naye Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shabani, alitaka kuongeza uzoefu na kupunguza changamoto ya masoko kwa wafanyabiashara.

Aliwataka pia wajasiriamali wote nchini kujisajili katika mamlaka na taasisi zilizomo katika wizara hiyo kwa lengo la kutambuliwa na kuwezeshwa kutumia vyema huduma zinazotolewa na taasisi hizo.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Islam Seif Salim, alisema tamasha hilo limepata maendeleo makubwa kutokana na kuongezeka kwa washiriki hadi kufikia 374 na miongoni mwao ni wa nje ya nchi.

# Wahamasishwa kuwahi chanjo kabla hazijapita muda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema kuwa dozi za chanjo ya corona zilizotumika ni 100,039 kati ya 300,000.

Aliyasema hayo wakati akijibu maswali ya waandishi wa habari wakati akizungumzia mafanikio ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya wizara yake.

Alisema wanatarajia kupata dozi zingine 200,000 kutoka China wakati wowote kuazia sasa na zingine za Pfizer kutoka Marekani wanatarajia kupokea mwezi huu.

Alisema chanjo ya corona kwa sasa imekuwa nyingi kuliko wachangaji kwa kuwa watu ni watu watu wenye mwamko wa kwenda kuchanja.

"Chanjo zikipita muda wake wa matumizi itabidi ziangamizwe na kuziangamiza kunahitaji fedha nyingi na utaalamu kwa hivyo shime wananchi mje mchanje," alisisitiza Mazrui.

Alisema katika kuendeleza mapambano hayo, serikali imekuwa ikitoa elimu ya afya kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwashajihisha kunawa mikono kwa sabuni mara kwa mara au kutumia vitakasa mikono, kuvaa barakoa na kujiepusha na misongamano isiyo ya lazima na kutoa chanjo ya corona ili kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema tangu Juni 17, 2021 katika vituo 36 vilivyoko wilayani vyenye kutoa chanjo aina ya Sinovac, Johnson & Johnson na Sputinik, takwimu zinaonyesha kwamba hadi kufikia Desemba 15, 2021 watu 138,139 sawa na asilimia 69.1 wameshapatiwa chanjo lengo ni kufikia watu 200,000.

Alikiri kuwa kuna tatizo la uhaba wa dawa katika vituo vya afya na hospitali za serikali na inachukua mzigo wa kutoa dawa muhimu kwa wananchi, lakini kutokana na uchumi wa nchi bajeti ya dawa si rahisi kufikia asilimia 100.

Alisema serikali ina mpango wa kuweka bima ya afya ili kupunguza mzigo kwa wale ambao hawana.

"Ni kweli kuna upungufu wa dawa, lakini jitihada ipo tumeanza na bilioni 16 hadi kufikia bilioni 22 kwa bajeti ya dawa, lakini hasa ukitaka dawa ambazo zitosheleze watu wote bajeti yake ni Sh. bilioni 62 hatunazo lazima twende katika bima ya afya ili kuipunguzia mzigo serikali katika suala la dawa," alisema Mazrui.

Alisema magonjwa yasiyoambukiza yameongezeka kwa kasi kubwa Zanzibar, na utafiti uliofanyika mwaka 2011 wa kuangalia tabia hatarishi zinazosababisha kupata maradhi hayo umeonyesha, kati ya watu waliofanyiwa utafiti asilimia 33 walikuwa na shindikizo la damu, asilimia 18 wana tabia ya kufanya mazoezi, asilimia 14.3 walikuwa na uzito uliopindukia na asilimia 24.5 walikuwa na lehemu (cholesterol) na hali hiyo si nzuri kiafya.

Waziri Mazrui alisema wizara yake inaendelea na ufuatiliaji wa kawaida wa magonjwa hayo katika hospitali na hadi kufika mwaka 2018, magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu, saratani na ajali za barabarani zilionekana kuripotiwa zaidi katika vituo vya afya.

"Idadi ya visa vipya vya magonjwa ya shinikizo la damu ilikuwa 19,271, kisukari 5,286, na visa 6,454 kwa ajali za barabarani," alisema.

Alisema katika kliniki ya magonjwa ya saratani hospitali ya Mnazi Mmoja, kumekuwa na ongezeko la wagonjwa waliothibitika kuwa na ugonjwa huo kutoka 336 mwaka 2020 na kufikia 392 kwa kipindi cha Januari hadi Novemba, 2021.

Alisema aina tano za saratani zinazoongoza, ni ya ubongo (103), mifupa (75), matiti (54), mlango wa kizazi (28) na tezi dume (26).

Alisema mafanikio mengine yaliyopatikana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ni kuanzisha huduma za matibabu ambazo hapo kabla zilikosekana na ni uchunguzi na matibabu ya saratani zilizoanza kutolewa mwaka 2016, usafishaji wa figo (mwaka 2017), ubongo na uti wa mgongo (mwaka 2014), uchunguzi za MRI (mwaka 2017) na upasuaji kwa kutumia njia za kisasa.

Alisema baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Wizara ya Afya iliendelea kuimarisha huduma za afya vijijini kwa kuongeza idadi ya vituo vya afya vya serikali 128 kutoka 44 vilivyokuwapo kabla ya Mapinduzi na kufikia jumla ya vituo vyote kuwa 172 (Unguja 98 na Pemba 74 kwa mwaka 2021.

# Aagiza wanaotoza wazazi kushughulikiwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, ameagiza walimu waliokuwa wakitoza fedha wazazi Sh. 50,000, kwa ajili ya kuandikisha wanafunzi kuanza shule, wafuatiliwe na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Mjema alibainisha hayo Ijumaa iliyopita, wakati wa utiaji saini mikataba 10 ya utekelezaji wa miradi ya maji mkoani humo, kati ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) na makandarasi, miradi yenye thamani ya Sh. bilioni 4.3.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akitafuta fedha na kuzielekeza kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ukiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa ili watoto wasome na elimu ni bure, lakini anasikitika kusikia wakati wa zoezi la uandikishaji wanafunzi kulikuwa na utozwaji wa fedha Sh.50,000.

"Mkoa wa Shinyanga katika fedha hizi za mapambano dhidi ya UVIKO-19, kwa upande wa ujenzi wa vyumba vya madarasa tulipata Sh. bilioni 17 na kujenga vyumba 393, ili watoto wetu wapate elimu na kutimiza ndoto zao, na madarasa yote yamekamilika na yamejengwa kwa ubora kabisa," alisema Mjema.

"Kutokana na ujenzi huu wa vyumba vya madarasa naomba watoto wote waende shuleni na kuhakikisha wanaandikishwa, na wale waliokuwa wakitoza wazazi Sh. 50,000 kwa ajili ya kuandikisha wanafunzi, naagiza watafutwe na kuchukuliwa hatua, na taarifa zao nizipate haraka wakiwa tayari wame adhibiwa," aliongeza.

Aidha, alisema haiwezekani Rais atoe agizo elimu ni bure, lakini wanatokea watu na kuanza kutoza wazazi fedha kwa ajili ya kuandikishwa wanafunzi, na kubainisha huo ni utovu wa nidhamu na lazima wapatiwe adhabu kali.

"Wakuu wa wilaya fuatilieni suala hili na watu hawa wachukuliwe hatua, Mheshimiwa Rais alishasema elimu ni bure, lakini wazazi wanaanza tena kutozwa fedha, lazima hili tulisimamamie ili kuimarisha nidhamu za watumishi wetu, RPC na TAKUKURU ukiona kuna mtu wa wako kwenye hili ukamshughulikie," alisisitiza Mjema.

Katika hatua nyingine Mjema, alisema serikali mkoani humo inaendelea kumpongeza Rais Samia, hivi karibuni atatoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji, pamoja na mbegu za muda mfupi, wakulima watakuwa wakilima mazao muda wote na kuondokana na tatizo la chakula.

Akizungumzia utekelezaji wa miradi 10 ya maji mkoani humo, aliwataka makandarasi ambao wamesaini mikataba hiyo, waitekeleze kwa ubora na thamani ya fedha ionekane, ili idumu kwa muda mrefu na kuhudumia vizazi na vizazi.

Kwa upande wake Meneja Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Juliety Payovela, alisema utekelezaji wa miradi hiyo 10 ya maji mkoani humo, itanufaisha wananchi 37,269 ambao wataondokana na adha kutumia maji machafu yasiyofaa kwa matumizi ya binadamu.

Naye Mkandarasi John Ntalimbo wa Kampuni ya JontaInvestment, akizungumza kwa niaba ya makandarasi wenzake, alimtoa wasiwasi Mkuu huyo wa Mkoa, kuwa miradi hiyo ya maji wataitekeleza kwa ubora unaotakiwa, pamoja na kuikamilisha kwa wakati.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, akizungumza katika kikao cha kamati ya mashauriano cha mkoa, kilichofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: ABDALLAH KHAMIS**

# Mil. 637/- zatengwa mkopo wajasiriamali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

HALMASHAURI ya Manispaa ya Kahama imetenga Sh. milioni 637 kwa ajili ya utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kama sehemu ya kutatua changamoto ya ukosefu wa mitaji.

Fedha hizo zimetengwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 na zinazotokana na mapato ya ndani. Hata hivyo, zimechelewa baada ya kuwapo kwa changamoto ya mfumo.

Halmashauri hiyo imezindua Baraza la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi ambalo litakuwa linashughulikia changamoto zinazowakabili hasa ukosefu wa mitaji, fursa za kibiashara na upatikanaji wa masoko ya uhakika ya ndani na nje ya Tanzania.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Robert Kwela, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa jukwaa hilo, lililoshirikisha wanawake watumishi wa umma na binafsi kuwa muda umefika kwa kundi hilo kubadilika na kujiingiza katika masuala ya kukuza uchumi wao.

Kwela alisema, halmashauri hiyo imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuwakopesha mikopo isiyokuwa na riba wajasiriamali vijana, kinamama na watu wenye ulemavu ili kuhakikisha wanakuwa kimtaji na kwamba fursa nyingine za mikopo zinapatikana katika taasisi za kifedha.

"Mwaka huu wa fedha tumetenga Sh. milioni 637 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, hivyo changamkieni fursa hii ili mkuze biashara zetu kwa kutanua wingi wa mitaji na masoko yenu," alisema Kwela.

Pia alisema, jukwaa hilo litasaidia kuwaunganisha wanawake wajasiriamali kupitia semina, makongamano mbalimbali na kupata fursa ya kufanya majadiliano hali ambayo itasaidia kukuza masoko ya biashara zao na mitaji waliyo nayo.

Akitoa taarifa ya uzinduzi wa jukwaa hilo, Hilda Robert alisema, kumekuwa na ubaguzi mkubwa wa kiuchumi baina ya makundi ya wanawake na wanaume na kusahau kuwa mwanamke ni kichocheo cha maendeleo nchini na kupewa kipaumbele cha mikopo kundi la wanaume.

Naye Mkuu wa Kituo cha Uwezeshaji Wananchi kiuchumi Kanda ya Ziwa, Jozaka Bukoku, alisema uanzishwaji wa majukwaa hayo ni mwogozo kutoka katika Baraza la Uwezeshaji la Taifa na wanajihusisha pia na kutoa programu za wanawake kwa wingi na hivi karibuni watawapatia elimu mama lishe.

## Upatikanaji maji Moro waongezeka

**Na Pauline Chimeledya,** MOROGORO

KIWANGO cha upatikanaji maji Mkoa wa Morogoro kimefikia asilimia 72 kutoka 69 hali inayosababisha kusuasua kwa upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha wadau wa maji kuhusu hali ya huduma ya maji mijini na vijijini mkoani humo, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, alisema, serikali imeupatia mkoa zaidi ya Sh. bilioni 14 kwa mwaka huu kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji. Alisema jumla ya miradi 30 itaanzishwa na kuboreshwa na kwamba fedha hizo ni ongezeko la asilimia 60 ikilinganishwa na bajeti ya zaidi ya Shilingi bilioni tisa ya mwaka uliopita.

Naye Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini mkoani humo (RUWASA), Mhandisi Msengi, alisema kuna miradi mbalimbali inaendelea na lengo ni kuwawezesha wananchi kupata huduma hiyo ya uhakika.

Naye Katibu Tawala wa mkoa huo, Mariam Mtunguja, aliitaka TARURA kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ili kuleta tija kwa wananchi wapate huduma muhimu ya maji, ikiwamo kudhibiti upotevu na matumizi mabaya ya fedha.

Kikao hicho kiliwakutanisha wataalamu wa maji wa mkoa na wilaya ikiwamo RUWASA, mamlaka za maji, wataalamu toka ofisi ya Bonde la Wami Ruvu, wabunge, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa wa Morogoro, makatibu tawala wa wilaya zote za mkoa, wenyeviti wa halmashauri zote, viongozi wa chama na wadau wa sekta ya maji.

## HABARI KIMATAIFA

# 22 wafariki dunia kwa theluji Pakistan

**Islamabad,** PAKISTAN

WATU 22 wamefariki dunia katika mji wa kitalii wa Kaskazini mwa Pakistan, baada ya kunasa kwenye magari yao usiku kucha, wakati wa kimbunga cha theluji.

Mwishoni mwa wiki, maelfu ya magari yalikwama katika mitaa mji wa kitalii, uliopo milima ya Muree.

Polisi wanadai baadhi ya waathirika huenda wamekufa kutokana na sumu ya kabonimonoksaidi kutokana na mabomba ya kutoa moshi ya magari yao kuzibwa na theluji.

Mji huo maarufu wa kitalii upo takribani kilomita 70 Kaskazini Mashariki mwa mji mkuu, Islamabad.

Licha ya tahadhari kutolewa na mamlaka, maelfu ya watu walijazana katika eneo hilo kuona theluji ikifunika mandhari.

Serikali imepeleka vikosi vya jeshi kwenye eneo la tukio, ili kuokoa watu ambao bado wamenasa katika takribani magari 1,000 na kuiondoa theluji barabarani. **NHK**



# Wanadiplomasia Marekani wajadili vikwazo vya Urusi ikiivamia Ukraine

**Geneva,** USWISI

MAZUNGUMZO kati ya Urusi na Marekani yanatarajia kuanza leo mjini Geneva, nchini Uswisi, yakiongozwa na Marekani huku tayari ikiwa na orodha ya vikwazo vilivyopangwa dhidi ya Moscow, kama itafanya uvamizi dhidi ya Ukraine.

Inasema ni vema kutuma ujumbe wa wazi kwa Vladimir Putin, kumwonya kabla ya kuanza kwa mazungumzo mjini Geneva.

Marekani na washirika wake wameandaa orodha ya vikwazo vya kijeshi, kiuchumi na kiteknolojia vilivyo tayari kutumika, endapo itatokea uvamizi dhidi ya Ukraine.

Nchi za Magharibi na Kiev, zinaishutumu Urusi kwa kuwakusanya wanajeshi wake karibu 100,000 kwenye mpaka wa Ukraine kwa nia ya uvamizi unaowezekana, baada ya Urusi kudhibiti Crimea, mwaka 2014.

**Usafirishaji wa bidhaa za watumiaji kama vile simu, kompyuta za Marekani pia zinapaswa kupigwa marufuku.**

Marekani na Ulaya wanataka kuondolewa kwa wanajeshi hao na kufufuliwa kwa mikataba ya Minsk, inayopaswa kumaliza mzozo wa Donbass, Mashariki mwa Ukraine, kati ya Kiev na waasi wanaoungwa mkono Urusi.

Moscow, kwa upande wake, inataka kukomeshwa kwa upanuzi wa NATO, kwenye milango yake na kupunguzwa kwa wanajeshi wa Muungano huo, Ulaya Mashariki. Madai ambayo yamefutiliwa mbali na wapinzani wake.

Vikwazo hivyo, vilivyofafanuliwa katika gazeti la New York Times na wanadiplomasia wa Marekani, ni pamoja na kutenga taasisi kuu za kifedha za Urusi kutoka soko la kimataifa, ili kudhoofisha uchumi moja kwa moja.

Pia kuzuia kuingia kwa huduma ya bomba la gesi la Nord Stream 2 ambalo ni muhimu kwa Kremlin.

Vikwazo vingine ni kufungia mauzo ya bidhaa za Marekani zinazotumiwa na viwanda mbalimbali vya Urusi, hasa viwanda muhimu kwa Vladimir Putin, kama vile vya silaha na anga za juu.

Usafirishaji wa bidhaa za watumiaji kama vile simu, kompyuta za Marekani pia zinapaswa kupigwa marufuku.

Marekani pia inapanga kuwapa raia wa Ukraine silaha za kupambana na wanajeshi wa Urusi, Marekani inatarajia kushawishi maamuzi ya rais wa Urusi.

Baadhi ya maofisa wanahofia kwamba Rais Putin, ataamua kuivamia Ukraine, ikiwa ataona mazungumzo ya Geneva hayakidhi matarajio yake. **RFI**



Mwanamume akionyesha noti ya paundi 100,000 ya Lebanon wakati wa maandamano dhidi ya kuporomoka kwa sarafu ya taifa hilo, mbele ya Benki Kuu 'Banque du Liban' mjini Beirut, juzi. **PICHA: XINHUA**

# Mchoro wa ramani wakutanisha waliyotengana kwa miongo 3

**Beijing,** CHINA

MWANAMUME mmoja ambaye alitekwa nyara kwa zaidi ya miaka 30 iliyopita, ameunganishwa tena na mama yake mzazi baada ya kuchora ramani ya kijiji chake cha utotoni kupitia kumbukumbu zake.

Li Jingwei, alikuwa na umri wa miaka minne tu aliposhawishiwa kutoka nyumbani kwao na kuuzwa katika kituo

Desemba 24, mwaka jana, alionyesha ramani iliyochorwa kwa mkono katika programu ya video, Douyin, ambayo polisi waliliganisha na kijiji kidogo na mwanamke ambaye mtoto wake wa kiume alitoweka.

Baada ya vipimo vya DNA, walikutanishwa tena katika kitongoji cha Yunnan Jumamosi wiki iliyopita.

Picha za video za kuungana kwao, zinawaonyesha wawili hao wakikutana kwa mara ya kwanza baada ya miongo mitatu.

"Miaka 33 ya kungoja, usiku mwingi wa kutamani na hatimaye ramani iliyochorwa kwa mkono kutokana na kumbukumbu, huu ni wakati mahususi wa kuachiwa baada ya siku 13," Li aliandika kwenye ukurasa wake wa Douyin kabla ya kukutana kwao.

"Asante, kila mtu ambaye amenisaidia kuungana na familia yangu."

Li, alitekwa karibu na mji wa Kusini Magharibi mwa Zhaotong katika kitongoji cha Yunnan, mwaka 1989 na baadaye akauzwa kwa familia iliyokuwa ikiishi umbali wa zaidi ya kilomita 1,800.

Sasa anaishi Guangdong, Kusini mwa China, hakufanikiwa kuwauliza wazazi, walezi waliomuasili au kutafuta hifadhi data za DNA kuhusu asili yake.

"Mimi ni mtoto ambaye natafuta nyumbani kwetu. Nilipelekwa Henan na jirani mwenye upara mwaka 1989, nilipokuwa na umri wa miaka minne," alisema kwenye video hiyo, ambayo imetumwa na maelfu kwenye mtandao.

"Hii ni ramani ya eneo la nyumbani kwangu ambayo nimeichora kutokana na kumbukumbu zangu," alisema akiinua ramani hiyo ya kijiji iliyochorwa ovyo, kulikuwa na vitu kama vile jengo ambalo aliamini kuwa ni shule, msitu wa mianzi na bwawa dogo.

Utekaji nyara wa watoto si jambo geni nchini China, jamii ambayo inathamini sana kupata mtoto wa kiume.

Watoto wengi hutekwa nyara wakiwa na umri mdogo na kuuzwa kwa familia nyingine. Mwaka wa 2015, ilikadiriwa kuwa watoto 20,000 hutekwa nyara kila mwaka.

Mwaka jana, kulikuwa na mifano mingi ya vijana waliounganishwa tena na wazazi wao wa kibaiolojia baada ya kutokuwa nao kwa muda mrefu.

Julai 2021, Guo Gangtang, aliunganishwa tena na mtoto wake wa kiume wa miaka 24, baada ya kutekwa nyara katika Jimbo la Shandong. **BBC**

# KIBU: NAPENDA KUCHEZA KAMA STRAIKA KULIKO WINGA

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa Timu ya Simba, Kibu Denis, amefichua kuwa hupenda zaidi kucheza na nafasi ya ushambuliaji kuliko winga.

Akizungumza akiwa mjini Zanzibar ambako timu yake inashiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi, Kibu amesema kuwa ingawa ana uwezo wa kucheza nafasi zote hizo kwa uwezo sawa, lakini anapenda zaidi kucheza kama straika.

"Nafasi zote mbili huwa nacheza na nacheza kwa usawa, hakuna inayonipa shida, ila ukiniambia napenda ipi zaidi nitakwambia kuwa ni straika kuliko winga," alisema Kibu ingawa hakutaka kufafanua zaidi.

**Kwenye mechi ya Ijumaa iliyopita dhidi ya Mlandege, mchezaji huyo kwanza alicheza nafasi ya winga wa kulia, lakini kipindi cha pili baada ya mabadiliko kadhaa alicheza kama mshambuliaji wa kati.**

Kibu, straika mwenye nguvu na mbio, kwa sasa amekuwa akiaminiwa na Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco.

Alisajiliwa msimu huu akitokea Mbeya City ambako alicheza kwa msimu mmoja tu, kabla ya hapo alikuwa timu ya Geita Gold wakati huo ikicheza Ligi Daraja la Kwanza, lakini kwa sasa ipo Ligi Kuu Tanzania Bara.

Viongozi wa Mbeya City walimwona kwenye mechi ya mchujo ('play off'), ilipocheza dhidi ya timu hiyo, pamoja na kufanikiwa kushinda na kusalia Ligi Kuu, lakini ikamchukua Kibu ambaye kwa sasa anatamba na Simba.




Mshambuliaji wa Simba Queens, Opah Clement, akimiliki mpira dhidi ya mabeki wa Yanga Princess kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara wakati timu hizo zilipokutana juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na Simba kushinda 4-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Opah, Masaka waanza mapema vita ya Kiatu*

**Na Adam Fungamwango**

WAFUMANIA nyavu tegemeo wa klabu za soka za wanawake, Opah Clement wa Simba Queens na Aisha Masaka (pichani) wa Yanga Princess wametambiana kila mmoja akidai kuwa ataibuka mfungaji bora wa Ligi Kuu ya Wanawake itakapomalizika.


Wakizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu baina ya timu hizo ambazo ni klabu pinzani na watani wa jadi, wachezaji hao kila mmoja amedai kuwa kutwaa Kiatu cha Dhahabu ni suala la muda tu.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba Queens, iliibabua Yanga Princess mabao 4-1, mawili yakifungwa na Opah, mengine yakifungwa na Mrundi Asha Jaffar, na bao la machozi la Yanga likifungwa kwa mkwaju wa penalti na Masaka.

"Mimi ni straika, kazi yangu ni kufunga mabao, nitakapopata nafasi mimi nafunga, na nategemea kuwa mfungaji bora msimu huu, hayo ndiyo malengo yangu," alisema Opah baada ya kumalizika mechi hiyo ambaye kwa sasa tayari ameshapachika mabao 10 kwenye mechi nne tu ambazo timu yake imecheza.

Naye Masaka ambaye mpaka sasa amefunga mabao sita kwenye ligi hiyo, ametamba kuwa ataibuka kuwa mfungaji bora, licha ya timu yao kupokea kichapo hicho cha mabao 4-1 kutoka kwa Simba Queens.

"Ingekuwa soka la wanaume kweli, lakini kwenye soka letu sisi wanawake, mabao manne ni machache sana, siku ukimpata kibonde, au timu haiko sawa sawa mnaifunga mabao mengi, na kama una uwezo wa kufunga unaweza kufunga hata mabao sita peke yako, kwa hiyo kupitwa mabao manne wala hainitishi," alisema Masaka ambaye ndiye kinara wa ufungaji msimu uliopita.



## Kocha Yosso Boys afunguka soka Znz

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Yosso Boys, Abdulrahaman Twalib, amesema ukosefu wa fedha unachangia kushuka na kupoteza mvuto wa soka la visiwani Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili visiwani hapa jana, Twalib alisema mpira ni pesa na watu wanawekeza katika soka ni ajira kwa wachezaji, lakini kwa visiwani humo imekuwa tofauti.

Alisema kwa mwenendo wa ligi ya visiwani humo, unafanya ligi yao kushuka chini kwa sababu wachezaji wanajitolea na kucheza kwa jihad kama ilivyo kwa Tanzania Bara.

"Kwa mwenendo wa soka letu la Zanzibar, tutakuwa wasindikizaji katika michuano ya Mapinduzi, miaka yote Simba, Yanga na Azam FC watakuwa watawala wa michuano hii kwa kila mwaka.

"Timu za Zanzibar haziwezi kushindanishwa na hizo za kutoka Bara, kwani zinapata huduma zote ikiwamo gym pamoja na wachezaji kulipwa mshahara mzuri, kwa hali hiyo mchezaji anapambana na kujituma hata akiumia anapata matibabu," alisema kocha huyo.

## Yanga yaonywa kwa Simba fainali

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

OFISA Habari wa Simba, Ahmed Ally, amesema endapo timu yao itakutana na Yanga kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi, anaamini kile walichokifanya dada zao, Simba Queens dhidi ya Yanga Princess, nao watakifanya.

Simba Queens juzi iliichapa Yanga Princess mabao 4-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Na kwa upande wa wanaume, Simba na Yanga leo zitashuka Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Namungo na Azam FC. Yanga itacheza dhidi ya Azam saa 10:15 alasiri wakati Simba ikivaana na Namungo saa 2:15 usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ahmed alisema kulingana na ubora wa kikosi chao, ana matumaini ya kufanya vizuri na kucheza fainali katika mchezo wao wa nusu fainali dhidi ya Namungo FC.

"Tuna wapongeza Simba Queens kufanya majukumu yao na kutuheshimisha, nina imani kama Azam FC wasipofanya majukumu yao ya kumwondoa Yanga basi watuachie sisi kwenye fainali, maana naziona zile 4-1, walizopokea dada zao," alisema Ahmed.

## ZISIKUPITE

### RONALDO MAMBO MAGUMU

WAKALA wa Cristiano Ronaldo, Jorge Mendes, 36, amesafiri kwenda England kwa ajili ya kukutana na mshambuliaji huyo wa Manchester United ambaye majaliwa yake klabuni hapo yapo shakani. ***(Sun)***

### HAALAND KUTUA MAN CITY

STRAIKA wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland, 21, anaamini kwamba, Manchester City itajaribu kumsajili kipindi cha majira ya joto, baada ya Manchester United kujiondoka kwenye mbio za kuwania saini ya nyota huyo. ***(Mario Cortegana via Express)***

### FERNANDES ATAKIWA BARCA

KIUNGO wa Manchester United na Ureno, Bruno Fernandes, 27, atawaniwa na Barcelona kama wakishindwa kumsajli Erling Haaland kipindi cha majira ya joto. ***(El Nacional, via Mail)***

### MORATA KUONDOKA JUVE

STRAIKA wa Hispania, Alvaro Morata, 29, anapanga kumaliza kipindi chake cha kucheza kwa mkopo Juventus ili ajiunge na Barcelona, lakini kocha, Massimiliano Allegri hana mpango wa kumwachia mchezaji huyo kabla ya kupata mrithi wake. ***(AS)***

### KEPA ATAKIWA LAZIO

LAZIO ina nia ya kutaka kumsajili golikipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga, 27, lakini mshahara wa nyota huyo wa pauni 170,000 kwa wiki unaweza kuwa kikwazo. ***(The Athletic)***

### KAMARA MSHAHARA MKUBWA

MLINZI wa Marseille, Boubacar Kamara, 22, anataka mshahara wa pauni 150,000 kwa wiki katika klabu mpya itakayomsajili huku West Ham ikiungana na Newcastle kuwania saini ya mchezaji huyo wa Ufaransa. ***(Sun).***

### TRAORE KUMRITHI DEMBELE

BARCELONA itamwania winga wa Wolves, Adama Traore, 25, kama mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24, ataamua kutoongeza mkataba mpya. ***(Diario Sport)***

### ATLETICO YAMTAKA SOARES

KLABU ya Atletico Madrid itataka kumsajili kwa mkopo beki wa kulia wa Arsenal, Cedric Soares, 30, huku ikiwa na nia ya kumpa mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto mchezaji huyo. ***(Mail)***


### VLAHOVIC KUAMUA FIORENTINA

STRAIKA wa Fiorentina na Serbia, Dusan Vlahovic, 21, anajiandaa kusubiri hadi kipindi cha majira ya joto ili kujua majaliwa yake. ***(90 Min)***

### BAILLY ATAKIWA MILAN

MLINZI wa Manchester United na Ivory Coast, Eric Bailly, 27, anawaniwa na AC Milan. ***(Sky Sports Italy, via Milan Live)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MSHAHARA WA DEMBELE WAELEZWA KUMTISHA XAVI

●●● Anataka pauni 700,000 kwa wiki na yupo katika nafasi nzuri ya kudai masilahi makubwa kutokana...

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi inasemekana aliachwa mdomo wazi alipojua kwamba Ousmane Dembele anataka mkataba utakaomfanya alipwe pauni 700,000 kwa wiki ili abaki pale Camp Nou.

Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa na wababe hao wa Catalunya unafika tamati mwishoni mwa Juni, na Barcelona wanapata kigugumizi kukubaliana na matakwa ya mkataba wa mshambuliaji huyo.

**Manchester United, Newcastle United na Liverpool wote wanaaminika kuwa na nia ya kumpeleka mshindi huyo wa Kombe la Dunia kwenye Ligi Kuu England kabla ya msimu wa 2022-23.**

Kwa mujibu wa mwandishi wa habari za michezo wa Ujerumani, Florian Plettenberg, madai ya mshahara wa Dembele ya pauni 700,000 kwa wiki yamemshtua Xavi, ambaye ameendelea kumuunga mkono Mfaransa huyo huku kukiwa na sintofahamu kuhusu mustakabali wake.

Mshambuliaji huyo yuko katika nafasi nzuri ya kudai mshahara mkubwa kutokana na hali ya mkataba wake, huku pia akiwa kwenye nafasi ya kupokea ada kubwa ya kusajiliwa kutoka kwa klabu mpya msimu huu wa majira ya joto.

Dembele amefunga mara moja na kutoa pasi mbili za mabao katika mechi tisa alizocheza katika ngazi ya klabu wakati wa msimu wa 2021-22.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
ASTON VILLA
1 | 1.75
X | 3.60
2 | 4.45

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BENZEMA APIGA BAO LA 300 REAL MADRID




**MADRID,** Hispania

STRAIKA wa Real Madrid, Karim Benzema, amefunga bao la 300 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo wakati wakitoka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Valencia Jumamosi kwenye Ligi Kuu Hispania.

Penalti aliyoifunga kabla ya mapumziko pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu lilimfanya nyota huyo wa Ufaransa kufikia idadi hiyo, kabla ya kufunga la pili dakika za majeruhi na kumfanya kufikisha mabao 22 katika mechi 25 msimu huu.

Benzema amefikisha idadi hiyo ya mabao katika mechi 584 alizoichezea Real Madrid na kumfanya kuwa mchezaji wa nne kufikisha idadi hiyo ya mabao kwenye historia ya klabu hiyo baada ya Cristiano Ronaldo (450), Raul (323) na Alfredo Di Stefano (308).

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alijiunga na Real Madrid akitokea Lyon mwaka 2009, na ameshinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, mara nne Klabu Bingwa Dunia, matatu ya La-Liga na mawili ya Copa del Rey.

Benzema alikuwa na mwaka mzuri 2021, akifunga mabao 30 kwa klabu yake katika mashindano yote akishinda pia taji la Ligi ya Mataifa ya Uefa akiwa na Ufaransa baada ya kuifunga Hispania mabao 2-1 kwenye fainali Oktoba.

## *Maguire: Wachezaji wanaimani na Rangnick*

**MANCHESTER,** England

HARRY Maguire amesisitiza kuwa wachezaji wa Manchester United wana "heshimu na kuamini" mbinu za Ralf Rangnick baada ya kikosi hicho kutokuwa na wakati mzuri kwenye Ligi Kuu England.


Ripoti za hivi karibuni zilibainisha kwamba wachezaji kadhaa wameonyesha kutoridhishwa na mbinu za Rangnick na kufikiria kuhusu majaliwa yao ya baadaye hapo Old Trafford.

Baada ya kuwa na mwanzo mbaya wa msimu, kulimfanya Ole Gunnar Solskjaer kutimuliwa Novemba na nafasi yake kuchukuliwa na raia huyo wa Ujerumani hadi mwishoni mwa msimu huu wa 2021-22.

Man United ilitoka sare ya bao 1-1 na Newcastle kabla ya mwaka mpya na ikafungwa 1-0 na Wolves nyumbani na kuibua malalamiko mengi.

Hata hivyo, Maguire anaamini kuwa wachezaji wa United wapo nyuma ya kocha huyo wa muda na amesema watafanya kila kitu wanachoweza kuhakikisha wanarudi kwenye ubora wao.

"Tunamheshimu na kuamini mbinu zake," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa England akiwaambia waandishi wa habari.



CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA



# DTB FC YAPANIA REKODI CHAMPIONSHIP



**Na Dennis Fussi**

KOCHA Mkuu wa DTB FC, Ramadhani Nsanzurwimo, ameweka wazi mikakati yake ni kuweka rekodi ya kutopoteza mechi yoyote kwa msimu huu wa Ligi ya Championship zamani Ligi Daraja la Kwanza.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Nsanzurwimo alisema wamecheza michezo 13 na hadi sasa hawajapoteza na anaendelea kukiimarisha kikosi chake hasa safu ya ulinzi kulinda lango lao.

Alisema anaendelea kuboresha safu yake ya ulinzi kuwa imara ili kutoruhusu kufungwa mabao lakini kuwapa mbinu washambuliaji wake za kutafuta ushindi hadi wanamaliza msimu.

"Ligi ya Championship ina ushindani mkubwa, tumecheza mechi 13 hatujafungwa, mipango yetu ni kuhakikisha tunapigania kuendelea na mwenendo huo wa kuzuia, tusipoteze mechi hadi tumalize ligi," alisema.

"Tunahitaji kuwa makini kwenye maandalizi yetu kwa kuhakikisha tunafanya vizuri katika kila mechi ili kufikia malengo ya timu kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao."

Kuhusu usajili, alisema utafanywa kulingana na mahitaji ya timu yao kwa kuongeza idadi ndogo ya wachezaji kutokana na mahitaji yakiwamo kuimarisha nafasi ya ulinzi na kiungo.

# Odhiambo atamba Prisons ikishusha mastraika wawili

**Dennis Fussi na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha mpya wa Tanzania Prisons, Patrick Odhiambo, akisema atatumia uzoefu na mbinu zake zote ili kuifanya timu hiyo kuwa bora msimu huu, uongozi wa timu hiyo umemshushia mastraika wapya wawili.

Odhiambo ambaye alikuwa akiinoa timu ya Biashara United, amesema Prisons ni moja ya timu nzuri na ina wachezaji wenye uwezo wa kupambana, hivyo anaamini kazi yake haitokuwa ngumu.

"Nafurahi kujiunga kwenye timu sahihi ambayo ina kila kitu ikiwamo wachezaji wazuri wenye uwezo, hapa kazi kwangu ni kuhakikisha narekebisha mapungufu yaliyopo ili turudi kwenye ushindani wa ligi," alisema Odhiambo.

Kocha huyo raia wa Kenya aliamua kuachana na Biashara United, baada ya uongozi wa timu hiyo kushindwa kuipambania timu katika masuala ya vibali vya wachezaji wapya ambao aliwasajili kutoka Kenya.

Katika hatua nyingine zikiwa zimebaki siku tano kabla ya kukamilika kwa dirisha dogo la usajili, klabu ya Prisons imesajili mastraika wawili, Aboubakar Malika kwa mkataba wa mwaka mmoja akitokea Mwadui FC, ambayo ipo Ligi ya Championship na Mudathir Said kutoka Coastal Union.





SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 10/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:45 | 3271 | AL Akhdood vs Ohud Medina | 2.75 | 2.90 | 2.56 |
| 16:00 | 1890 | Sheffield Wednesday U23 vs Coventry U23 | 3.13 | 3.86 | 1.92 |
| 16:00 | 5036 | Millwall U23 vs Charlton U23 | 1.77 | 3.85 | 3.61 |
| 16:00 | 5383 | Senegal vs Zimbabwe | 1.39 | 4.35 | 8.11 |
| 16:00 | 5748 | Crewe U23 vs Hull City U23 | 2.98 | 3.80 | 1.99 |
| 17:00 | 5453 | Mumbai City FC vs Bengaluru FC | 1.99 | 3.47 | 3.23 |
| 17:30 | 1634 | Aston Villa U23 vs Middlesbrough U23 | 1.75 | 3.94 | 3.65 |
| 17:40 | 3141 | AL Nahdha vs AL Jeel | 2.25 | 3.08 | 3.03 |
| 17:40 | 4674 | Al Shabab Kuwait vs AL Tadamon | 2.51 | 3.09 | 2.65 |
| 17:45 | 1221 | Hajer Club vs Alshoulla | 2.74 | 2.79 | 2.65 |
| 17:45 | 1699 | AL Khalidiyah vs Najma Manama | 1.63 | 3.42 | 5.20 |
| 17:45 | 1845 | AL Badii vs East Riffa | 3.66 | 3.23 | 1.94 |
| 18:00 | 5127 | Doxa Katokopia vs Pafos FC | 2.93 | 3.22 | 2.39 |
| 19:00 | 2426 | Guinea vs Malawi | 1.56 | 3.61 | 6.53 |
| 19:00 | 4290 | Morocco vs Ghana | 2.09 | 3.07 | 3.76 |
| 19:00 | 5402 | Benfica Lisbon B vs Porto B | 2.37 | 3.52 | 2.64 |
| 19:00 | 5549 | Torino vs Fiorentina | 2.90 | 3.35 | 2.40 |
| 19:55 | 2761 | AL Qadsia vs AL Nasr | 1.38 | 4.53 | 6.55 |
| 20:00 | 1791 | Omonia Nicosia vs Olympiakos Nicosia | 1.60 | 3.87 | 5.36 |
| 20:00 | 1829 | Hapoel Petah Tikva vs Hapoel Afula | 2.38 | 3.08 | 3.08 |
| 20:00 | 1987 | Ironi Hasharon vs Sectzya Nes Ziona | 3.71 | 3.27 | 2.02 |
| 20:00 | 2953 | Altinordu vs Keciorengucu | 2.89 | 3.23 | 2.25 |
| 20:00 | 3278 | Fenerbahce vs Adana Demirspor | 1.80 | 3.60 | 4.15 |
| 20:00 | 4556 | Maccabi Bney Reine vs SC Kfar Qasem | 2.97 | 2.97 | 2.52 |
| 20:20 | 3388 | Manama Club vs Riffa Club | 2.60 | 3.23 | 2.46 |
| 20:45 | 4758 | Jong Utrecht vs Jong Ajax | 3.81 | 4.00 | 1.75 |
| 21:00 | 4367 | Nacional Madeira vs CD Feirense | 1.97 | 3.41 | 3.51 |
| 21:15 | 1622 | Bnei Sakhnin vs Hapoel Katamon | 1.90 | 3.17 | 3.85 |
| 22:00 | 1092 | Derby County U23 vs Liverpool U23 | 1.52 | 4.43 | 4.62 |
| 22:00 | 1477 | Comoros vs Gabon | 3.72 | 3.03 | 2.12 |
| 22:00 | 1685 | Burnley U23 vs Birmingham U23 | 1.85 | 3.86 | 3.33 |
| 22:00 | 1710 | Everton U23 vs Crystal Palace U23 | 3.41 | 3.85 | 1.83 |
| 22:00 | 2225 | Stoke City U23 vs Norwich U23 | 1.90 | 3.86 | 3.18 |
| 22:00 | 3297 | West Ham U23 vs Leeds United U23 | 2.07 | 3.70 | 2.89 |
| 22:00 | 4184 | Newcastle U23 vs West Bromwich U23 | 2.29 | 3.93 | 2.44 |
| 22:00 | 4266 | Manchester United U23 vs Tottenham U23 | 1.84 | 3.94 | 3.32 |
| 22:00 | 5646 | Nottingham U23 vs Fulham U23 | 3.75 | 3.95 | 1.72 |
| 22:00 | 5664 | Sunderland U23 vs Reading U23 | 1.99 | 3.67 | 3.09 |
| 22:45 | 4704 | Bradford PA vs Gateshead | 5.01 | 4.04 | 1.53 |
| 22:45 | 5644 | Toulouse vs Nancy | 1.46 | 4.22 | 6.28 |
| 22:55 | 1191 | Manchester Utd vs Aston Villa | 1.75 | 3.60 | 4.45 |
| 23:00 | 1734 | Real Oviedo vs Eibar | 2.31 | 3.09 | 3.09 |
| 23:00 | 2050 | Jong PSV vs Almere City | 2.33 | 3.37 | 2.79 |
| 23:00 | 2199 | Espanyol vs Elche | 1.85 | 3.50 | 4.30 |
| 23:15 | 2868 | Gil Vicente vs Vitoria Guimaraes | 2.52 | 3.16 | 2.77 |

JUMANNE - 11/01/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 4860 | Shabab AL Ahli Dubai Club vs AL Khaleej Khor Fakkan | 1.63 | 3.57 | 4.83 |
| 17:00 | 5118 | Jamshedpur vs East Bengal | 1.50 | 4.15 | 5.22 |
| 17:40 | 4197 | Al Salmiyah vs Kazma SC | 2.60 | 3.45 | 2.60 |
| 18:30 | 1493 | Jazira Abu Dhabi vs Al Wasl Dubai | 2.03 | 3.18 | 3.42 |
| 22:45 | 2044 | Cagliari vs Bologna | 2.85 | 3.30 | 2.46 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Januari 10, 2022
Nipashe



Mshahara wa Dembele wamtisha Xavi

UKURASA 21



## Nyota 10 kutazamwa Fainali za Afcon 2022

**YOUNDE,** Cemroon

MICHUANO ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2022, ilianza jana Jumapili nchini...

HABARI UK. 12

## Kibu afunguka nafasi anayopenda kucheza



Na Adam Fungamwang

MCHEZAJI wa Timu ya Simba, Kibu Denis, amefichua kuwa hupenda zaidi kucheza...

HABARI UK. 20



PAPE SAKHO MAYELE

# SIMBA, YANGA ZAANZA KUTAFUTANA MAPINDUZI

●●● Pablo awataja waamuzi akiimulika Namungo kwanza, mastaa wa Jangwani wawahi Z'bar kwa...

**Saada Akida na Hawa Abdallah,**

ZANZIBAR

WAKATI miamba ya soka nchini Simba na Yanga ikishuka dimbani leo kwenye mechi za nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi visiwani hapa, sasa ni dhahiri makocha wa timu hizo wameanza kutafutana ili kuonyesha nani zaidi baada ya kila mmoja kueleza dhamira yake ya kutinga fainali na kutwaa taji hilo.

**Michezo miwili ya nusu fainali ya michuano hiyo itapigwa leo katika Uwanja wa Amaan, ambapo Yanga itavaana na Azam FC majira ya saa 10:15 alasiri huku Simba ikiwa na shughuli pevu dhidi ya Namungo saa 2:15 usiku.**

Akizungumzia mchezo wao wa leo dhidi ya Namungo, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, jana alisema anaamini utakuwa mgumu lakini mzuri wakutazama kwa kuwa timu zote zinaweka mpira chini, hivyo kilichobaki ni waamuzi kutenda haki kwa kufuata sheria zote 17 za soka bila kuwalinda wanaocheza rafu mbaya hasa zile zinazohatarisha afya za wachezaji.

"Utakuwa mchezo mgumu, Namungo ni moja ya timu nzuri, ila tunaamini itakuwa mechi bora ya kutazama kwa kuwa timu zote zinacheza soka na si vurugu.

"Katika michuano inapofika hatua kama hii, kila mechi inakuwa ngumu, lakini tumejiandaa kwa hilo kwa kuwa tunataka kushinda taji hili," alisema Pablo.

Lakini kwa Yanga ambayo hii itakuwa mara yao ya pili kukutana na Azam FC hatua ya nusu fainali baada ya mwaka jana kuwatoa 'Wanalambalamba' hao kwa mikwaju ya penalti 4-3 kwenye hatua kama hiyo, wamepania tena kufanya kweli leo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Makipa wa Yanga, Razak Siwa, alisema wamejiandaa kufanya vizuri na kuna baadhi ya wachezaji wameungana na wenzao kikosini na huenda wakaonekana katika mchezo huo wa leo.

Hata hivyo, Nipashe jana lilishuhudia wachezaji wa timu hiyo ambao hawakuwapo awali, Saido Ntibazonkiza, Yanick Bangala na Fiston Mayele, wakiwa mazoezini jana na wenzao katika Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

"Tumejiandaa vizuri dhidi ya Azam FC kwetu haituumizi kichwa kwa sababu tumezoea kuifunga, kikubwa tunatakiwa kujipanga vizuri kuhakikisha tunaenda kucheza fainali ya Mapinduzi," alisema Siwa.

Kocha wa makipa wa Azam FC, Iddi Abubakar kwa upande wake, alisema wamejiandaa vizuri na wanaiheshimu Yanga kwa sababu mwaka jana waliwatoa kwa penalti, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu ya kuwaogopa.

"Hatuingia kulipa kisasi, tutacheza mpira na tunaenda kwa mbinu nyingine kabisa, pia tutamkosa Shaban Chilunda ambaye ni majeruhi," alisema Iddi.

Fainali ya michuano hiyo ambayo mwaka huu zilijumuisha timu 10, sita za Zanzibar na nne kutoka Tanzania Bara, itapigwa Alhamisi wiki hii na ikitarajiwa kukutanisha timu zote za Bara baada ya zile za visiwani zote kushindwa kufuzu nusu fainali.

Timu za Zanzibar ambazo michuano hiyo imekuwa mlima mrefu kwao mwaka huu ni KMKM, Taifa Jang'ombe, Mlandege FC, Yosso Boys , Selem View na Meli Nne City, huku za kutoka Tanzania Bara ambazo zote zimetinga hatua ya nusu fainali ni Simba, Yanga, Azam pamoja na Namungo FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042